

Maoni yaliyotolewa katika ripoti hii ni ya waandishi na si lazima yaakisi maino ya Shirika la Uhamiaji wa Kimataifa (IOM). Majina yaliyotumiwa na uwasilishaji wa nyenzo katika ripoti yote havikusudii kutoa maoni yoyote upande wa IOM kuhusu hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, wilaya, mji au eneo, au mamlaka yake, au kuhusu maeneo yake ya mipakani au mipaka yake.

IOM imejitolea kutekeleza kanuni kwamba uhamiaji wa kibinadamu na wenye utaratibu hunufaisha wahamiaji na jamii. Kama shirika lisilo la serikali, IOMhufanya kazi na washirika wake katika jamii ili: kusaidia katika kukabiliana na changamoto za kusimamia uhamiaji; uelewaji wa mapema wa masuala ya uhamiaji; kuhimiza maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia uhamiaji; na kudumisha hadhi ya utu na ustawi wa wahamiaji.

---

Mchapishaji: Shirika la Kimataifa la Uhamiaji
17 route des Morillons
P.O. Box 17
1211 Geneva 19
Switzerland
Simu: +41 22 717 9111
Faksi: +41 22 798 6150
Baruapepe: hq@iom.int
Tovuti: www.iom.int

Picha ya Jalada: Wengi wa wakimbizi na wahamiaji zaidi ya 300,000 wa Venezuela wanaovuka mpaka wa Ecuador na Colombia hupita katika eneo hili la mpaka huko Ipiales, Columbia. Wengine hupitia kwenye vizuizi vilivyoimarishwa, au njia zisizo rasmi na zilizo hatari sana, katika maeneo ya mashambani kupitia milimani na kuvuka mito ili kuingia Ecuador. © IOM 2019/Muse Mohammed

Marejeo Yanayohitajika: International Organization for Migration (IOM), 2021. Migration and migrants: A global overview. In: *World Migration Report 2022* (M. McAuliffe and A. Triandafyllidou, eds.). IOM, Geneva.

---

ISBN 978-92-9268-385-6 (PDF)

**© IOM 2022**

Baadhi ya haki zimehifadhiwa. Kazi hii inapatikana chini ya Creative Commons Attribution-NonCommercial-NoDerivs 3.0 IGO License (CC BY-NC-ND 3.0 IGO).*

Kwa maelezo zaidi tafadhali tazama Hakimiliki na Masharti ya Matumizi.

Chapisho hili halipaswi kutumiwa, kutolewa au kusambazwa upya kwa madhumuni ambayo kimsingi yamekusudiwa au yanaelekezwa kwa faida ya kibiashara au kujipatia fedha, ila tu kwa madhumuni ya elimu k.m. kujumuishwa katika vitabu vya kiada.

Ruhusa: Maombi ya matumizi ya kibiashara au haki zaidi na utoaji leseni yanapaswa kuwasilishwa kwa publications@iom.int.

* https://creativecommons.org/licenses/by-nc-nd/3.0/igo/legalcode

PUB2022/082/L

# 2 UHAMIAJI NA WAHAMIAJI: MUHTASARI WA HALI DUNIANI

## Utangulizi

Lazima kueleza na kuchanganua jinsi uhamiaji unavyobadilika duniani kutoka kwa mitazamo mbalimbali, ikijumuisha ile inayohusisha vipimo vya kiuchumi, kijamii na kiusalama (na mifumo ya sera na sheria inayohusiana nayo), kuanze na uelewa wa vipimo vya kimsingi. Uhamiaji wa binadamu unaweza kuwa ni shughuli ya zamani inayogusa karibu kila jamii duniani; hata hivyo, inabadilika kwa njia muhimu. Kuchunguza mabadiliko ya kiwango, mwelekeo, demografia na idadi ya matukio kunaweza kuonyesha jinsi uhamiaji unavyobadilika huku pia kukiashiria mienendo ya muda mrefu ambayo imetokana na matukio ya kihistoria na pia ya hivi majuzi.

Makadirio ya sasa ulimwenguni ni kwamba kulikuwa na takribani wahamiaji milioni 281 wa kimataifa duniani kote katika mwaka wa 2020, idadi ambayo ni sawa na asilimia 3.6 ya watu duniani.[1] Jambo la kwanza muhimu la kutambua ni kwamba hiki ni kikundi kidogo cha idadi ya watu duniani, na hii ina maana kwamba kuishi katika nchi aliyozaliwa mtu ndilo jambo la kawaida kwa wengi. Watu wengi hawahami kuvuka mipaka; wengi zaidi huhama ndani ya nchi.[2] Baada ya kusema hayo, ibainike kwamba makadirio haya yanahusiana na wahamiaji, wala sio matukio ya uhamaji. Ugonjwa tandavu wa UVIKO-19 umeangazia uhusiano uliopo baina ya uhamiaji na mwendo, huku vikwazo vya kusafiri vilivyoletwa na UVIKO-19 vikisababisha kiasi kikubwa cha ukosefu wa mwendo duniani kote. Wakati wa kuandika makala hii (Julai 2021), vikwazo vya usafiri katika nchi nyingi vilikuwa vinawekwa (kurudishwa tena) au kuimarishwa wakati virusi vya aina mbalimbali vikienea uliwenguni, na kuujaribu uthabiti wa pamoja wa ulimwengu katika kukabiliana na tatizo la kiafya la kimataifa ambalo halijawahi kuonekana katika karne iliyopita.

Wakati taratibu za uhamaji zisipozuiwa na magonjwa tandavu duniani, idadi kubwa ya watu huhama kimataifa kwa sababu zinazohusiana na kazi, familia na masomo – ikihusisha michakato ya uhamiaji ambayo hufanyika kwa kiasi kikubwa bila kuwapa changamoto wahamiaji au nchi wanazoingia. Kinyume chake ni kwamba watu huondoka kwenye makazi na nchi zao kwa sababu mbalimbali za lazima na wakati mwingine za kuhuzunisha, kama vile vita, mateso na maafa. Wakati wale ambao wamefurushwa, kama vile wakimbizi na watu waliohamishwa ndani ya nchi (IDPs), ni asilimia ndogo ya wahamiaji wote, mara nyingi wao ndio huhitaji zaidi usaidizi na uungwaji mkono.

Sura hii, inayoangazia data na mienendo muhimu ya uhamiaji duniani, pamoja na data mpya ya UVIKO-19 ya uhamaji na inayohusiana na usafiri, inalenga kuwasaidia watunga sera, weledi na watafiti katika kuelewa hali nzima ya uhamiaji, kwa kutoa muhtasari wa hivi punde wa uhamiaji na wahamiaji duniani. Sura hii inategemea vyanzo vya hivi punde vya takwimu zilizokusanywa na Idara ya Masuala ya Kiuchumi na Kijamii ya Umoja wa Mataifa (UN DESA), Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD), Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO), Benki ya Dunia, Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Wakimbizi (UNHCR), Kituo cha Ufuatiliaji wa Wakimbizi wa Ndani (IDMC),

1 UN DESA, 2021a.

2 Makadirio ya hivi karibuni yalikuwa wahamiaji wa ndani milioni 740 duniani kote katika mwaka wa 2009 (UNDP, 2009).

Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) na Chuo Kikuu cha Oxford.[3] Sura hii inatoa muhtasari wa data na mienendo ulimwenguni kuhusu wahamiaji wa kimataifa (idadi yao) na uhamaiaji wa kimataifa (mtiririko). Pia inatoa mjadala wa makundi mahususi ya wahamiaji – yaani, wafanyikazi wahamiaji, wakimbizi, waomba hifadhi, wakimbizi wa ndani ya nchi na wahamiaji waliopotea – pamoja na utumaji wa pesa kimataifa na vikwazo vya usafiri vinavyohusiana na UVIKO-19.

Sura hii pia inarejelea mkusanyiko wa data za kiprogramu za IOM, hasa kuhusu ufuatiliaji wa usaidizi wa kurejea nyumbani kwa hiari na ujumuishaji tena katika jamii, utoaji wa makazi mapya na ufurshwaji.[4] Ingawa data hizi kwa jumla si za ulimwengu mzima au kiwakilishi chake, zinaweza kutoa utambuzi wa mabadiliko ambayo yametokea katika upangaji husika na oparesheni duniani kote. Kama shirika la Umoja wa Mataifa la uhamiaji, lenye shughuli zinazohusiana na mada zote zilizojadiliwa katika sura hii, data za IOM zina uwezo wa kutoa ufahamu zaidi juu ya uhamiaji na mienendo yake anuwai, ikiwa ni pamoja na mahitaji tofauti ya wahamiaji.

### Kufafanua uhamiaji, mhamiaji na istilahi zingine muhimu

Mbali na ufafanuzi wa jumla wa *uhamiaji* na *wahamiaji*, kama ule unaopatikana katika kamusi, kuna ufafanuzi anuwai mahususi wa istilahi muhimu zinazohusu uhamiaji, ukijumuisha nyanja za sheria, utawala, utafiti na takwimu.[a] Ingawa hakuna ufafanuzi uliokubaliwa ulimwenguni wa uhamiaji na mhamiaji, fasili kadhaa zinakubaliwa na wengi na zimekuzwa katika mazingira mbalimbali, kama zile zilizoelezwa katika *Mapendekezo kuhusu Takwimu za Uhamiaji wa Kimataifa* ya UN DESA 1998.[b] Kazi imekamilishwa hivi majuzi na Kitengo cha Takwimu cha Umoja wa Mataifa na kikosi kazi cha Kundi la Wataalamu la Umoja wa Mataifa kuhusu Takwimu za Uhamiaji juu ya mfumo wa dhana uliorekebishwa kuhusu takwimu za uhamiaji na mwendo ili kuongoza mchakato unaoendelea katika kusasisha Mapendekezo ya 1998.[c] Kiunzi hicho cha dhana kiliidhinishwa na Tume ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa katika kikao chake cha 52 mnamo Machi 2021, kikifungua njia kwa mapendekezo yaliyorekebishwa kuhusu mhamiaji na mwendo wa kimataifa ambao unaweza kueleza vyema vipengele tofauti vya mwendo, ikiwa ni pamoja na uhamiaji.[d] Kiunzi hicho cha dhana kimeelezwa kwa muhtasari katika Kiambatisho A.

Ufafanuzi wa kiufundi, dhana na kategoria za wahamiaji na uhamiaji kwa kawaida huongozwa na masuala ya kijiografia, kisheria, kisiasa, kimethodolojia, kiwakati na mengineyo. Kwa mfano, matukio ya uhamiaji yanaweza kufafanuliwa kwa njia nyingi, pamoja na kuyahusisha na mahali pa kuzaliwa, uraia, mahali pa kuishi na muda wa kukaa mahali.[e] Hili ni muhimu wakati wa kupima na kuchambua athari za uhamiaji na wahamiaji, vyovyote zilivyofafanuliwa. Tunawahimiza wasomaji kurejelea vyanzo vya msingi vilivyotajwa katika sura hiyo kwa habari kuhusu ufafanuzi mahususi na uainishaji msingi wa data. Wasomaji wanaweza pia kupata kuwa IOM *Glossary on Migration* (toleo la 2019) ni rejeleo linalofaa. *Faharasa* hiyo inapatikana katika Jukwwaa la Machapisho ya IOM: https://publications.iom.int/books/international-migration-law-ndeg34-glossary-migration.

a Tazama, kwa mfano, Poulain na Perrin, 2001.
b UN DESA, 1998.
c Kitengo cha Takwimu cha Umoja wa Mataifa, 2021.
d Tume ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa, 2021.
e Tazama, kwa mfano, de Beer et al., 2010.

3 Ili kusalia katika mawanda ya ripoti hii, takwimu zilizotumika katika sura hii zilikuwa za hivi punde zaidi kufikia tarehe 30 Juni 2021, isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo.

4 Data za IOM kuhusu waathiriwa wa biashara haramu ya binadamu zimewasilishwa katika Sura ya 10 ya ripoti hii.

## Wahamiaji wa kimataifa: idadi na mienendo

UN DESA hutoa makadirio ya idadi ya wahamiaji wa kimataifa ulimwenguni. Majadiliano yafuatayo yanatumia makadirio hayo, ambayo yanategemea data iliyotolewa na Mataifa.[5] *Mapendekezo ya* Umoja wa Mataifa *Kuhusu Takwimu za Uhamiaji wa Kimataifa* ya sasa yanafafanua "mhamiaji wa kimataifa" kama mtu yeyote ambaye amebadilisha nchi yake ya makazi ya kawaida, yakitofautisha kati ya "wahamiaji wa muda mfupi" (wale ambao wamebadilisha nchi zao za makazi ya kawaida kwa angalau miezi mitatu, lakini chini ya mwaka mmoja) na "wahamiaji wa muda mrefu" (wale ambao wamefanya hivyo kwa angalau mwaka mmoja). Hata hivyo, si nchi zote zinatumia ufafanuzi huu kiutendaji.[6] Nchi zingine hutumia vigezo tofauti kutambua wahamiaji wa kimataifa, kwa mfano, kutumia vipindi tofauti vya muda mfupi zaidi vya makazi. Tofauti kati ya dhana na ufafanuzi, na pia njia za kukusanya data baina ya nchi, huzuia ulinganifu kamili wa takwimu za kitaifa kuhusu wahamiaji wa kimataifa. Mapitio ya mapendekezo ya Umoja wa Mataifa yanaendelea kwa sasa, kama ilivyojadiliwa katika kijisanduku cha maandishi hapo juu.

Idadi inayokadiriwa ya wahamiaji wa kimataifa imeongezeka katika miaka hamsini iliyopita. Katika mwaka wa 2020, karibu watu milioni 281 waliishi katika nchi tofauti na nchi zao za kuzaliwa, au karibu milioni 128 zaidi ya ilivyokuwa miaka 30 iliyopita, katika mwaka wa 1990 (milioni 153), na zaidi ya mara tatu ya idadi iliyokadiriwa katika mwaka wa 1970 (milioni 840). Uwiano wa wahamiaji wa kimataifa kama sehemu jumla ya idadi ya wahamiaji duniani imeongezeka, lakini taratibu tu. Idadi kubwa ya watu wanaishi katika nchi ambayo walizaliwa. Ni vigumu kutathmini athari ya UVIKO-19 kwa wahamiaji wa kimataifa duniani. Sababu moja ya hali hii ni kwamba data ya hivi karibuni zaidi inayopatikana ni ya katikati mwa 2020,[7] ambapo ni mwanzoni mwa ugonjwa huu tandavu. Baada ya kusema hayo, inakadiriwa kuwa huenda UVIKO-19 imepunguza idadi ya wahamiaji wa kimataifa kwa karibu milioni mbili. Kwa maneno mengine, kama UVIKO-19 haingekuwepo, idadi ya wahamiaji wa kimataifa katika mwaka wa 2020 ingekuwa karibu milioni 283.[8]

### Jedwali la 1. Wahamiaji wa kimataifa, 1970–2020

| Mwaka | Idadi ya wahamiaji wa kimataifa | Wahamiaji kama % ya idadi ya watu ulimwenguni |
|---|---|---|
| 1970 | 84 460 125 | 2.3 |
| 1975 | 90 368 010 | 2.2 |
| 1980 | 101 983 149 | 2.3 |
| 1985 | 113 206 691 | 2.3 |
| 1990 | 152 986 157 | 2.9 |
| 1995 | 161 289 976 | 2.8 |
| 2000 | 173 230 585 | 2.8 |
| 2005 | 191 446 828 | 2.9 |
| 2010 | 220 983 187 | 3.2 |
| 2015 | 247 958 644 | 3.4 |
| 2020 | 280 598 105 | 3.6 |

*Chanzo*: UN DESA, 2008; UN DESA, 2021a.
*Kumbuka*: Idadi ya asasi (kama vile Mataifa, wilaya na maeneo ya kiutawala) ambazo data yake ilitolewa katika Idadi ya Wahamiaji wa Kimataifa ya UN DESA 2020 ilikuwa 232. Mnamo 1970, idadi ya asasi ilikuwa 135.

5 Data inatolewa pia na wilaya na maeneo ya kiutawala kwa UN DESA. Kwa muhtasari wa vyanzo vya data vya idadi ya UN DESA, mbinu na tahadhari, tafadhali tazama UN DESA, 2021b.


6 UN DESA, 1998.

7 UN DESA, 2021b.

8 UN DESA, 2021c.

Wakati idadi ya wahamiaji wa kimataifa inapochunguzwa na ukanda wa Umoja wa Mataifa, kwa sasa Ulaya ndipo mahali ambapo wahamiaji wengi wa kimataifa huenda, ikiwa na wahamiaji milioni 87 (30.9% ya wahamiaji wote wa kimataifa), ikifuatwa kwa karibu na wahamiaji wa kimataifa milioni 86 wanaoishi Asia (30.5%).[9] Wahamiaji wa kimataifa milioni 59 (20.9%) huelekea Amerika Kaskazini, ikifuatwa na Afrika yenye wahamiaji milioni 25 (9%). Katika kipindi cha miaka 15 iliyopita, idadi ya wahamiaji wa kimataifa huko Amerika ya Kusini na Karibiani imeongezeka zaidi ya mara mbili kutoka karibu milioni 7 hadi milioni 15, na kuufanya kuwa ukanda wenye kiwango cha juu sana cha ukuaji wa wahamiaji wa kimataifa na unaopokea asilimia 5.3 ya wahamiaji wote wa kimataifa. Takriban wahamiaji milioni 9 wa kimataifa wanaishi Oceania, au karibu asilimia 3.3 ya wahamiaji wote. Ukuaji wa wahamiaji wa kimataifa wanaoishi katika kila ukanda kati ya 2005 na 2020 umeonyeshwa kwenye Kielelezo cha 1.

## Kielelezo cha 1. Wahamiaji wa kimataifa, kulingana na ukanda mkuu wa makazi, 2005–2020 (milioni)




*Chanzo*: UN DESA, 2021a.


Oceania ina idadi kubwa zaidi ya wahamiaji wa kimataifa kama kiwango cha idadi jumla ya watu, huku asilimia 22 ya watu wote wakiwa wamezaliwa katika nchi nyingine. Amerika Kaskazini ina idadi ya pili kwa ukubwa ya wahamiaji wa kimataifa wakiwa asilimia 15.9, ikifuatwa na Ulaya kwa asilimia 11.6. Amerika ya Kusini na Karibiani, Afrika, na Asia zina idadi za asilimia 2.3, 1.9. na 1.8 mtawalia.

Kama ilivyokuwa miaka 50 iliyopita, Marekani panabaki kuwa mahali ambapo wahamiaji wengi zaidi huelekea, ikiwa na zaidi ya wahamiaji wa kimataifa milioni 51. Ujerumani imekuwa nchi ya pili kwa umashuhuri wanakoelekea wahamiaji, ikiwa na karibu wahamiaji wa kimataifa milioni 16, huku Saudi Arabia ikiwa nchi ya tatu kwa wingi wa wahamiaji wa kimataifa inaowapokea, wakiwa milioni 13. Shirikisho la Urusi na Uingereza zinakamilisha nchi tano bora wanakoelekea wahamiaji, zikiwa na wahamiaji wa kimataifa milioni 12 na 19 mtawalia. Orodha ya nchi 20 wanakopenda kwenda wahamiaji inaweza kupatikana katika paneli ya kushoto ya Kielelezo cha 2.

9 UN DESA, 2021a.

Ikiwa na karibu watu milioni 18 wanaoishi nje ya nchi, India ina idadi kubwa zaidi ya wahamiaji duniani, na hili linaifanya kuwa nchi wanakotoka wahamiaji wengi zaidi duniani kote. Meksiko ni nchi ya pili iliyo asili ya wahamiaji wengi wakiwa karibu milioni 11. Shirikisho la Urusi ni nchi asili ya tatu kwa ukubwa, ikifuatwa kwa karibu na Uchina (karibu milioni 10.8 na milioni 10 mtawalia). Nchi ya tano iliyo asili kubwa ya wakimbizi ni Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, yenye zaidi ya watu milioni 8 wanaoishi nje ya nchi, hasa kama wakimbizi kutokana na ufurushwaji mkubwa uliotokea muongo mmoja uliopita (tazama majadiliano yaliyo katika sehemu ya wakimbizi hapo chini). Paneli iliyo upande wa kulia katika Kielelezo cha 2 inaonyesha nchi 20 zilizoongoza kama vyanzo vya wahamiaji katika mwaka wa 2020.

Kielelezo cha 2. Nchi 20 zinazowapokea wahamiaji wengi wa kimataifa (kushoto) na nchi wanazotoka (kulia) mnamo 2020 (milioni)






*Chanzo*: UN DESA, 2021a.

### Jukwaa la Kuonyesha Data ya Uhamiaji Duniani

Mnano Mei 2021, IOM ilizindua wavuti mpya wa Ripoti ya Uhamiaji Duniani ambayo inaunganisha simulizi za uhamiaji zenye msingi wa ukweli na taswira shirikishi za data kuhusu data na mienendo iliyosasishwa zaidi ya uhamiaji duniani.[a]




Umbo hili la kidijiti linatoa uwakilishi angavu wa data kwa kuonyesha taswira ya mwingiliano wa mienendo ya uhamiaji duniani. Kwa kuzingatia uchanganuzi ulioandaliwa katika ripoti, tovuti hiyo hutoa takwimu na ramani za uhamiaji katika kiwango cha nchi, taswira shirikishi ya njia za uhamiaji, na nchi zinazoongoza katika kutuma na kupokea pesa tangu mwaka wa 1995, pamoja na data ya kimataifa na kikanda. Vipengele vipya shirikishi kuhusu vizuizi vya UVIKO-19 viliongezwa kutoka kwa ripoti hii ya sasa.


Kwa kutayarisha muktadha wa taswira ya habari, taswira ya data inapendelea ufahamu unaoeleweka zaidi wa ukubwa wa idadi na mienendo iliyopo, ikijaliza uchanganuzi wa kina uliowasilishwa kwenye ripoti hiyo. Jukwaa hili la mwingiliano linapatikana kwa Kiingereza, Kifaransa na Kihispania.

a IOM, 2020a.

Data inayopatikana ya wahamiaji wa kimataifa inajumuisha makadiro ya uhusiano wa wanakotoka na wakoelekea kati ya nchi mbili, ili kuwezesha ukadiriaji wa "njia" za uhamiaji kati ya nchi mbili duniani kote. Ukubwa wa njia za uhamiaji kutoka nchi A hadi nchi B hupimwa kwa idadi ya watu waliozaliwa katika nchi A ambao walikuwa wanaishi katika nchi B katika mwaka wa 2020. Njia za uhamiaji huwakilisha mkusanyiko wa safari za uhamiaji za muda mrefu na hutoa picha ya haraka ya jinsi ruwaza za uhamiaji zimebadilika na kuwa idadi kubwa ya watu waliozaliwa nje ya nchi wanaoishi katika nchi mahususi walizohamia.

Kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo cha 3, njia ya Meksiko hadi Marekani ndiyo kubwa zaidi duniani ikiwa na takriban watu milioni 11. Njia ya pili ni ile inayotoka Jamhuri ya Kiarabu ya Syria hadi Uturuki, inayojumuisha hasa wakimbizi waliofurushwa kutoka kwa makazi yao kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe katika Jamhuri ya Kiarabu ya Syria vilivyodumu kwa muongo mmoja. Kwa upande mwingine, njia ya tatu kwa ukubwa duniani, kutoka India hadi Milki za Kiarabu (zaidi ya milioni 3), inajumuisha hasa wahamiaji wafanyikazi. Njia ya nchi mbili kati ya Shirikisho la Urusi na Ukraine huchukua nafasi za nne na tano miongoni mwa njia kubwa zaidi ulimwenguni. Takriban watu milioni 3 waliozaliwa katika Shirikisho la Urusi sasa wanaishi Ukraine, huku karibu idadi sawa ya watu wamehama kutoka Ukraine hadi Shirikisho la Urusi.

Kielelezo cha 3. Njia 20 maarufu za uhamiaji wa kimataifa kutoka nchi moja hadi nyingine, 2020





Chanzo: UN DESA, 2021a.
*Kumbuka*: Njia hizi zinawasilisha idadi ya wahamiaji wa kimataifa (milioni) waliozaliwa katika nchi iliyotajwa kwanza na wanaoishi katika nchi ya pili. Njia huwakilisha mkusanyiko wa safari za uhamiaji kwa muda mrefu na hutoa picha ya haraka ya jinsi ruwaza za uhamiaji zimebadilika na kuwa idadi kubwa ya waliozaliwa nje ya nchi wanaoishi katika nchi mahususi walizohamia.

Wahamiaji wengi wa kimataifa (karibu 78%) walikuwa na umri wa kufanya kazi (kati ya miaka 15 na 64). Tangu mwaka wa 1990, mgao wa wahamiaji wa kimataifa wenye umri wa miaka 19 na chini umepungua kutoka asilimia 18.9 hadi 14.6, huku wahamiaji wa kimataifa wenye umri wa zaidi ya miaka 64 wamesalia bila kubadilika kwa karibu asilimia 12.2.

Kwa sasa kuna idadi kubwa ya wahamiaji wa kimataifa wanaume kuliko wanawake duniani kote, na tofauti hiyo imeongezeka katika kipindi cha miaka 20 iliyopita. Katika mwaka wa 2000, mgawanyiko wa wanaume kwa wanawake ulikuwa asilimia 50.6 hadi 49.4 (au wahamiaji wa kiume milioni 88 na wahamiaji wa kike milioni 86). Katika mwaka wa 2020 mgawanyiko ulikuwa asilimia 51.9 hadi 48.0, huku wahamiaji wa kiume wakiwa milioni 146 na wahamiaji wa kike wakiwa milioni 135. Mgao wa wahamiaji wa kike umekuwa ukipungua tangu mwaka wa 2000, huku mgao wa wahamiaji wa kiume ukiongezeka kwa asilimia 1.4. Tazama Kielelezo cha 4 kwa uainishaji wa kijinsia.

Kielelezo cha 4. Wahamiaji wa kimataifa, kijinsia, 2000–2020




*Chanzo*: UN DESA, 2021a.

## Kuunganisha “uhamiaji” na “mhamiaji”

Kwa jumla, **uhamiaji** ni mchakato wa kuondoka sehemu moja kwenda nyingine. Kuhamia ni kuondoka, iwe kutoka eneo la mashambani kwenda jijini, kutoka wilaya au mkoa mmoja katika nchi maalumu hadi wilaya au mkoa mwingine katika nchi hiyo hiyo, au kutoka nchi moja kwenda nchi mpya. Inahusu vitendo.

Kinyume chake, **mhamiaji** ni mtu anayeelezwa hivyo kwa sababu moja au nyingi, kulingana na muktadha (tazama kisanduku cha maandishi kuhusu “Kufafanua uhamiaji, mhamiaji na istilahi zingine muhimu” hapo juu). Ingawa katika visa vingi, “wahamiaji” huhusika na aina fulani ya uhamiaji, hili halitokei wakati wote.

Katika hali zingine, watu ambao hawajawahi kuhamia wanaweza kuitwa wahamiaji - kwa mfano, watoto wa watu waliozaliwa ng’ambo kwa kawaida huitwa wahamiaji wa kizazi cha pili au cha tatu.[a] Hili linaweza hata kujumuisha hali zinazohusu kutokuwa na utaifa, ambapo vikundi vyote vya watu haviwezi kupata uraia licha ya kuzaliwa na kukulia katika nchi hiyo. Watu kama hao wanaweza hata kurejelewa na serikali kama wahamiaji wasio halali.[b]

a Tazama, kwa mfano, Neto, 1995; Fertig na Schmidt, 2001.
b Kyaw, 2017.

## Mtiririko wa uhamiaji wa kimataifa


Huku data kuhusu idadi ya wahamiaji wanaoishi mahali fulani ikipatikana kwa urahisi, data kuhusu safari za uhamiaji ulimwenguni (mtiririko = idadi ya wahamiaji wanaoingia au kutoka eneo fulani) ni ndogo zaidi. Makadirio ya UN DESA kuhusu wahamiaji ulimwenguni ni mapana na yametanda duniani kote; hata hivyo, hifadhidata ya mtiririko wa wahamiaji inahusisha nchi 45 pekee.[10] Kupata data ya mtiririko wa wahamiaji kuna changamoto nyingi kwa sababu kadhaa. Kwanza, wakati mtiririko wa wahamiaji wa kimataifa unakubaliwa kwa ujumla kuwa unajumuisha wanaoingia na kutoka katika nchi, kumekuwepo na umakini mkubwa katika kurekodi wanaoingia. Kwa mfano, wakati nchi kama vile Australia na Marekani zinahesabu watu wanaovuka mpaka wa kimataifa kutoka na kuingia, nchi zingine nyingi zinahesabu tu wanaoingia na wala si wanaoondoka.[11] Zaidi ya hayo, data ya wahamiaji wanaoingia na kutoka katika baadhi ya nchi hutokana na matukio ya kiutawala yanayohusiana na hali ya uhamiaji (kwa mfano, utoaji/usasishaji/uondoaji wa kibali cha makazi) na kwa hivyo hutumiwa kama kiwakilishi cha mtiririko wa uhamiaji. Zaidi ya hayo, mara nyingi ni vigumu kutenganisha safari za uhamiaji na safari zisizo za uhamiaji, kama vile utalii au biashara.[12] Pia kufuatilia safari za uhamiaji kunahitaji rasilimali nyingi, miundombinu na mifumo ya teknolojia ya habari/maarifa. Hili linaleta changamoto mahususi kwa nchi zinazoendelea, ambapo uwezo wa kukusanya, kusimamia, kuchambua na kuripoti data ya usafiri, uhamiaji na maeneo mengine mara nyingi huwa mdogo. Mwishowe, jiografia za nchi nyingi zinazua changamoto kubwa kwa kukusanya data juu ya mtiririko wa uhamiaji. Usimamizi wa vituo vya kuingia nchini na mipaka, kwa mfano, una changamoto kubwa katika baadhi ya kanda, kwa sababu ya mipaka ya funguvisiwa na iliyojitenga, na inafanywa kuwa changamano zaidi na desturi za uhamiaji usio rasmi kwa ajili ya kazi.[13]

Hivi sasa kuna hifadhidata kuu mbili za kimataifa juu ya mitiririko ya uhamiaji wa kimataifa, ambazo zote zinatokana na takwimu za kitaifa: Seti ya Data ya Mtiririko wa Uhamiaji wa Kimataifa ya UN DESA na Hifadhidata ya Uhamiaji ya Kimataifa ya OECD. Tangu mwaka wa 2005, UN DESA imekusanya data juu ya mtiririko wa wahamiaji wa kimataifa kwenda na kutoka nchi zilizochaguliwa, kulingana na takwimu zinazopatikana kitaifa. Wakati wa kuandika ripoti hii (Julai 2021), hakukuwepo na sasisho kwa seti ya data ya mtiririko ya UN DESA, huku toleo la hivi punde zaidi likiwa la 2015. Hesabu ya mitiririko ya uhamiaji ya 2015 inajumuisha data kutoka nchi 45, likiwa ongezeko kutoka nchi 29 katika mwaka 2008 na nchi 15 katika mwaka wa 2005.[14]

OECD imekuwa ikikusanya data ya mtiririko wa uhamiaji wa kimataifa tangu mwaka wa 2000, ikiruhusu uchanganuzi wa mwenendo kufanywa juu ya kikundi kidogo cha nchi kuu wanakoelekea wahamiaji, kama ilivyoonyeshwa katika Kielelezo cha 5 (ingawa data haijafanywa kuwa wastani, kama ilivyoelezewa katika maelezo yaliyo chini ya kielelezo). Takwimu za hivi punde zaidi zinaonyesha kuwa katika mwaka wa 2018, ongezeko la asilimia 10 la mtirirko wa uhamiaji wa kudumu lilirekodiwa kutoka mwaka uliotangulia wa 2017. Marekani, mojawapo ya nchi kuu wanakokwenda wahamiaji, ilipokea takriban wahamiaji wapya milioni 1.1 katika mwaka wa 2018, hii ikiwa ni punguo ya asilimia 2.7 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Nchi nyingine ambayo ilipata mabadiliko makubwa ilikuwa Chile, ikiwa na ukuaji wa asilimia 64. Kuhusiana na nchi za Ulaya zilizo katika OECD, uhamiaji kwa ujumla uliongezeka kwa karibu 136,000 katika mwaka wa 2018 (3.2% zaidi kuliko 2017). Ndani ya Ulaya, Uingereza na Italia zilipata punguo la 6.5 na 5.2 mtawalia katika mtiririko wa kudumu. Badala yake, ukuaji huko Ulaya uliongozwa na Uhispania (+23%, au ongezeko la karibu 106,000) na Ureno (+52%, au ongezeko la karibu 32,000).

10 UN DESA, 2015.
11 Koser, 2010; McAuliffe na Koser, 2017.
12 Skeldon, 2018.
13 Gallagher na McAuliffe, 2016.
14 Kwa data ya mtiririko wa uhamiaji ya UN DESA, na pia kwa nchi mahususi zilizojumuishwa, tafadhali tazama UN DESA, 2015.

Kielelezo cha 5. Uingiaji wa raia wa kigeni katika nchi za OECD, uhamiaji wa kudumu, 2000-2018 (milioni)




*Chanzo*: OECD, n.d.a.

*Kumbuka*: Data hazijasawazishwa kwa hivyo zinatofautiana na takwimu za mtiririko ndani wa wahamiaji katika nchi zilizochaguliwa zilizo katika mfululizo wa OECD wa International Migration Outlook. Nchi 35 ambazo kwa kawaida hujumuishwa katika takwimu za OECD ni zifuatazo: Australia, Austria, Ubelgiji, Canada, Chile, Czechia, Denmark, Estonia, Ufini, Ufaransa, Ujerumani, Ugiriki, Hungary, Iceland, Ireland, Israel, Italia, Japan, Latvia, Luxembourg, Meksiko, Uholanzi, New Zealand, Norway, Poland, Ureno, Jamhuri ya Korea, Slovakia, Slovenia, Uhispania, Uswidi, Uswizi, Uturuki, Uingereza na Marekani. Kwa miaka kadhaa, data ya nchi fulani haitolewi: data iliyotolewa ilikuwa ya nchi 31 katika mwaka 2000. Hasa, data ya Ugiriki haikuripotiwa kati ya mwaka 2000 na 2004, na data ya Uturuki iliripotiwa tu katika miaka 2010, 2016, 2017 na 2018.

Athari za UVIKO-19 kwa usafiri duniani kote zimejadiliwa hapa chini katika sura hii na pia katika Sura ya 5 ya ripoti hii.

### *Mtiririko wa uhamiaji usio salama*

Baadhi ya njia za uhamiaji huleta changamoto nyingi zaidi kuliko zingine, kwa wahamiaji na vilevile kwa wenye mamlaka. Wakati mwingine safari za wahamiaji zinaweza kuwa na matokeo yasiyo salama na yaliyo hatari, mara nyingi yanayohusisna na msururu wa masuala ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kimazingira na kisera ambayo yanaweza kuathiri pakubwa jinsi watu wanavyohamia.[15] Kufuatia matukio ya kusikitisha ya Oktoba 2013, ambapo zaidi ya watu 360 walikufa boti mbili zilipozama karibu na kisiwa cha Italia cha Lampedusa, IOM ilianza kukusanya na kuweka pamoja taarifa za wahamiaji wanaoangamia au kupotea katika njia za wahamiaji duniani kote kama sehemu ya Mradi wake wa Wahamiaji Waliopotea.[16] Vyanzo vya data vinajumuisha rekodi rasmi za walinzi wa pwani na wakaguzi wa kitabibu, visa vya vyombo vya habari, ripoti kutoka kwa mashirika yasiyo ya serikali na mashirika ya Umoja wa Mataifa, na mahojiano na wahamiaji.[17]


15 McAuliffe et al., 2017.

16 Tazama https://missingmigrants.iom.int/.

17 IOM, n.d.

Katika kipindi cha miaka sita ya ukusanyaji wa data, mwaka wa 2020 ulikuwa na jumla ya chini kabisa (takribani 3,900), ukilinganishwa na takribani 5.400 zilizopatikana katika mwaka uliotangulia wa 2019 (tazama Kielelezo cha 6). Kupungua kwa vifo kati ya 2019 na 2020 kunaakisi, kwa sehemu, vizuizi vya usafiri vilivyowekwa kwa sababu ya ugonjwa tandavu wa UVIKO-19. Kuna uwezekano kwamba 2021 pia itarekodi idadi ya vifo iliyopungua kwa jumla, kwa sababu vizuizi vya usafiri vinaendelea ulimwenguni. Kwa jumla, kati ya 2014 na 2020, Bahari ya Mediterania imeshuhudia idadi kubwa ya vifo, ikihusika katika vifo vya zaidi ya watu 21,200. Katika mwaka wa 2020, Bahari ya Mediterania iliendelea kuwa mahali penye idadi kubwa zaidi ya vifo wakati wa uhamiaji, ikiwa na zaidi ya vifo 1,460. Kufuatia mwenendo ulioonekana katika miaka sita iliyopita, kulikuwa na kiwango kikubwa cha vifo kwenye "njia ya Mediterania ya Kati".[18]

Kielelezo cha 6. Vifo vya wahamiaji kikanda, 2014–2020




*Chanzo*: IOM, n.d. (imepitiwa tarehe 20 Septemba 2021).
*Kumbuka*: Data inajumuisha vifo vilivyorekodiwa na vilevile wale walioripotiwa kupotea. Tazama wavuti wa Mradi wa Wahamiaji Waliopotea kwa utondoti wa mbinu na kanda za kijiografia (https://missingmigrants.iom.int/).

Mradi wa Wahamiaji Waliopotea unakabiliwa na changamoto kubwa katika ukusanyaji wake wa data. Kwa mfano, vifo vingi vilivyorekodiwa ni vya watu wanaosafiri kupitia njia za siri, ambazo mara nyingi huwa baharini au katika maeneo ya mbali (ili kukwepa kutambuliwa), na hii ina maana kwamba mara nyingi maiti hazipatikani. Kuna vyanzo rasmi vichache vinavyokusanya data kuhusu vifo vya wahamiaji na kuiweka hadharani. Kutegemea ushuhuda wa wahamiaji wenzako na vyanzo vya vyombo vya habari kunaweza kuwa tatizo kutokana na matangazo yasiyo sahihi na kamili. Hata hivyo, mradi huu unatoa mwanga juu ya mada ambayo hapo awali haikufanyiwa utafiti wa kutosha na ilipuuzwa, na hivyo kuweka wazi haja ya kushughulikia suala hili la kusikitisha linaloendelea, ikiwa ni pamoja na katika muktadha wa utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji Salama, Uliopangwa na Halali.

18 Ibid.

### *Athari za UVIKO-19 kwa usafiri*

UVIKO-19 umekuwa ugonjwa tandavu mkali zaidi katika karne moja, huku maambukizi yake ya juu, aina tofauti za virusi na ukali wa ugonjwa vikiwaingiza watunga sera katika eneo geni. Ingawa msisitizo umekuwa katika kukabiliana na msukosuko wa afya duniani (k.m. upimaji wa virusi, kutibu magonjwa, na ukuzaji wa chanjo na upangaji wa programu) sehemu ya juhudi za kukabiliana nao imehusisha mabadiliko makubwa ya uhuru wa watu kwenda popote duniani, jambo ambalo nalo limeathiri pakubwa usafiri wa binadamu duniani. Kutosafiri kunakohusiana na UVIKO-19 kumekuwa "kivurugaji" kikubwa cha uhamiaji.[19]

Serikali kote ulimwenguni zilitekeleza hatua mbalimbali za kupunguza maenezi ya virusi hivyo, na vikwazo vingi vilianzishwa kutoka mwanzoni mwa 2020, vikibadilika jinsi wakati ulivyosonga. Seti mpya za data ziliibuka ili kufuatilia mwitikio wa sera duniani kote, kama vile Kifuatilia Mwitikio wa Serikali kuhusu UVIKO-19 cha Chuo Kikuu cha Oxford,[20] ambacho kimerekodi majibu mengi ya serikali kote duniani, kama vile hatua za "kutotoka nyumbani", kufungwa kwa mahali pa kazi, kufungwa kwa shule, vikwazo kuhusu mikusanyiko, vikwazo kuhusu usafiri wa ndani ya nchi, na hatua za udhibiti wa usafiri wa kimataifa. Zaidi ya hayo, IOM ilianza kufuatilia vikwazo vya usafiri duniani kote ugonjwa huu tandavu ulipoanza, ikitumia data mbalimbali na kuripoti matokeo kupitia dashibodi yake ya Athari za UVIKO-19 kwa Usafiri.[21] Tazama data, utafiti na uchanganuzi wa ziada katika Sura ya 5 yenye maudhui ynayohusu athari za UVIKO-19 katika ripoti hii.

Baadhi ya nchi, kama vile El Salvador, Israel, New Zealand, Nigeria, Qatar na Singapore, ziliweka kwa haraka vikwazo muhimu vya usafiri wa kimataifa (kufikia mwanzoni mwa Machi 2020), huku zingine zikichukua hatua wiki au miezi kadhaa baadaye.[22] Baadhi ya nchi zilisitisha uingiaji wote wa raia wa kigeni, zingine zilipiga marufuku raia wa nchi mahususi, na zaidi ya hayo, nchi zingine zilifunga mipaka kabisa ili kuzuia kuondoka na kuingia kwa watu wote, ikiwa ni pamoja na raia wao wenyewe.[23] Pia hatua za karantini zilianzishwa na baadhi ya nchi, zikihitaji abiria wanaoingia katika nchi wawekwe karantini wakiwa wamejitenga kwa muda fulani (kwa kawaida siku 10 hadi 14) mara tu wanapowasili.

Kwa jumla, hatua za vizuizi vya kusafiri za UVIKO-19 – za ndani na za kimataifa – ziliwekwa haraka na idadi kubwa ya nchi ulimwenguni kote, huku kilele kikitokea mwishoni mwa Machi hadi mwanzoni mwa Aprili 2020 (tazama Kielelezo cha 7). Ingawa kulikuwa na uwezekano mkubwa wa kuweka vikwazo vya kusafiri kimataifa ugonjwa huu tandavu ulipoanza, kulikuwa na hatua mbalimbali za udhibiti wakati wa wiki za mwanzo (pamoja na kupimwa mapema), labda kwa sababu serikali ilihitaji kutathmini uzito wa tatizo hilo katika kipindi cha wasiwasi mkubwa. Ukali wa UVIKO-19 ulipodhihirika, idadi ya vikwazo vya usafiri wa kimataifa na wa ndani iliongezeka sana.

---

19 McAuliffe, 2020.


20 Hale et al., 2021.

21 Tazama https://migration.iom.int/.

22 Hale et al., 2021.

23 IOM, 2020b; *Al Jazeera*, 2020.

## Kielelezo cha 7. Vidhibiti vya usafiri vinavyohusiana na UVIKO-19: kimataifa na ndani ya nchi, Januari 2020–Juni 2021, nchi zote




*Chanzo*: Hale et al., 2021.
*Maelezo*: Kategoria zilizotumika ni zile za Kifuatilia Mwitikio wa Serikali cha Oxford; kategoria zilizojumuishwa katika seti ya data ni za vikwazo vinavyohusiana na UVIKO-19 pekee na hazionyeshi vikwazo vingine vya usafiri ambavyo vinaweza kuwa vimewekwa, kama vile vinavyohusiana na vizuizi vya visa, marufuku ya kuingia kwa msingi wa uraia, vikwazo vya kuondoka/kutoka na vikwazo vya usafiri wa ndani.


Tofauti za mabadiliko ya vikwazo zinaweza kuonekana katika Kielelezo cha 7, ambacho kinaonyesha kuwa vikwazo vya usafiri wa kimataifa vya aina fulani vinavyohusiana na UVIKO-19 vilikuwa bado vinatekelezwa katika nchi zote ulimwenguni mwaka mmoja baada ya tangazo la Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusu ugonjwa huo tandavu tarehe 10 Machi 2020.[24] Kinyume chake, vikwazo vya ndani vilipungua baada ya muda. Baada ya kusema hayo, kuna mambo matatu muhimu ya kusisitiza kutoka kwenye data hii:

- Ingawa kuna vikwazo vya usafiri wa kimataifa vya aina fulani katika nchi zote, kuna mchanganyiko wa kupimwa, karantini na marufuku (jumla/mahususi);
- Zaidi ya nusu ya nchi zote zilikuwa bado zina marufuku ya kusafiri (jumla au mahususi) mwaka mmoja baada ya ugonjwa huu tandavu kuanza;
- Zaidi ya theluthi moja ya nchi zote zilikuwa bado zina vizuizi vya usafiri wa ndani mwaka mmoja baada ya ugonjwa huo tandavu kuanza.

24 WHO, 2020.

Vikwazo vya kimataifa vinavyohusiana na UVIKO-19 vinapochunguzwa baada ya muda, tunaweza kuona kwamba vikwazo vya usafiri/mipaka na hatua zinazohusiana na afya vimebadilika kadri teknolojia na uwezo wa ugavi unaosaidia hatua zinazohusiana na afya zinavyoanzishwa na kutekelezwa. Upimaji wa kabla ya kusafiri, karantini na uingiaji unaoidhinishwa na chanjo unaotolewa na nchi tofauti ulishuhudia vikwazo vya usafiri vikipitwa na hatua zinazohusiana na afya mnamo Oktoba 2020.

Kielelezo cha 8. Hatua za usafiri wa kimataifa zinazohusiana na UVIKO-19: Machi 2020–Juni 2021, nchi zote





*Chanzo*: IOM, 2021a.

*Kumbuka*: Ni nchi pekee (si wilaya) zimejumuishwa katika uchanganuzi huu. Hatua zinazohusiana na afya zinajumuisha uchunguzi na ufuatiliaji wa afya, vyeti vya kupima/matibabu, na hatua za karantini. Vizuizi vya usafiri vinajumuisha vizuizi vya abiria kulingana na utaifa au kuwasili kutoka eneo fulani la kijiografia. Tazama ukurasa wa vikwazo vya usafiri vya DTM kwa maelezo zaidi kuhusu mbinu.

Athari za vikwazo vya usafiri vinavyohusiana na UVIKO-19 huwa wazi sana wakati data ya abiria wa ndege inapochunguzwa. Tunaweza kuona kutokana na takwimu za muda mrefu za abiria wa ndege kwamba vikwazo vya usafiri wa UVIKO-19 vilikuwa na athari kubwa kwa usafiri wa ndege wa kimataifa na wa ndani katika mwaka wa 2020. Jumla ya abiria waliobebwa ilishuka kwa asilimia 60 kutoka kama bilioni 4.5 katika mwaka wa 2019 hadi bilioni 1.8 katika mwaka wa 2020 (Kielelezo cha 9).

Kielelezo cha 9. Abiria wa ndege wanaobebwa duniani kote, 1945–2020




*Chanzo*: ICAO, 2021.

Kwa ujumla, tunaweza kuona kwamba UVIKO-19 imekuwa na athari kubwa kwa usafiri, na hivyo kwa uhamiaji, huku vikwazo vikisalia kwa muda mrefu kuliko wengi walivyotarajia, hali iliyosababishwa kwa kiasi fulani na changamoto zinazoletwa na aina za virusi zinazoibuka na "mawimbi" ya maambukizi yanayotokea. Bado athari za muda mrefu hazijaeleweka kikamilifu, lakini uchanganuzi ulioelezwa katika Sura ya 5 unaonyesha mabadiliko ya uhamiaji na usafiri katika maeneo kadhaa muhimu.

## UVIKO-19 na wahamiaji waliokwama

Vizuizi vya usafiri vilivyowekwa wakati wa UVIKO-19 vilisababisha matatizo makubwa kwa baadhi ya wahamiaji na kuzidisha mazingira magumu yaliyopo. Kufungwa kwa mipaka kulikwamisha maelefu ya wahamiaji, wakiwemo wafanyikazi wa muda, wamiliki wa hati za makazi ya muda, wanafunzi wa kimataifa, wahamiaji wanaosaifiri kutafuta matibabu, wanufaishwa wa msaada wa kurejea nyumbani na ujumuishwaji tena katika jamii, mabaharia na wengine.

Kufikia katikati ya mwaka wa 2020, vizuizi vinavyohusiana na ugonjwa huo tandavu vilikuwa vimewakwamisha karibu watu milioni 3 nje ya nchi zao, wengi wao wakiwa ni wasafiri wa mara kwa mara kama vile wafanyikazi wahamiaji, wanafunzi na watalii. Wengi wa wasafiri hawa waliachwa bila huduma za ubalozi, ikiwa ni pamoja na usaidizi wa hadhi yao kisheria katika nchi hiyo, na wengine hawakuwa na pesa za kutosha ili kulipia chakula na malazi. Wengi walikuwa Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini (takribani milioni 1.3), zikifuatwa na Asia na Pasifiki (takribani 977,000).

Masuala mahususi yaliyowakabili wahamiaji hawa yalitofautiana sana, kama ilivyokuwa kwa hali zao, lakini kwa ujumla, changamoto zilikuwa za aina mbili. Kwanza zilikuwa zinazohusiana na masuala ya usafiri. Haya yalihusiana na kutosonga kulikotokana na vikwazo vya dharura vya uchukuzi na usafiri. Changamoto zingine kubwa zilikuwa gharama na mchakato uliohusika katika kurejea nyumbani. Zaidi ya hayo, ukosefu wa ushirikiano kati ya nchi za asili, nchi wanakohamia na nchi za mpito ulizidisha matatizo ya usafiri.

Pili kulikuwa na mazingira magumu yaliyohusishwa na hadhi ya uhamiaji ya wahamiaji. Hadhi hii inaweza kuzuia uwezekano wa kupata usaidizi kutoka kwa serikali, hali ambayo iliwaweka watu kwenye, au kuwaweka katika hatari ya, umaskini uliokithiri. Mazingira mengine magumu yalijumuisha chuki dhidi ya wageni na unyanyapaa, kukwama kwa watu baharini, na kuongezeka kwa hatari ya kiafya kwa wale wanaoishi katika makazi yenye msongamano wa watu na/au wale wasioweza kufikia programu za chanjo ya UVIKO-19.


*Vyanzo*: IOM, 2020c; Benton et al., 2021.

## Wafanyikazi wahamiaji

Makadirio ya hivi karibuni yanayopatikana yanaonyesha kwamba kulikuwa na takribani wafanyikazi wahamiaji milioni 169 ulimwenguni kote katika mwaka wa 2019, wakisimamia karibu theluthi mbili (62%) ya milioni 272 ya (wakati huo) idadi ya wahamiaji wa kimataifa duniani.[25] Inafaa kukumbuka kwamba makadirio haya yalikuwepo kabla ya UVIKO-19, ambayo imeathiri uhamiaji wa wafanyikazi kimataifa kwa njia nyingi, ingawa inatoa vipimo ambavyo athari za UVIKO-19 zinaweza kutathminiwa dhidi yake katika siku zijazo.[26] Ikilinganishwa na idadi ya wahamiaji wa kimataifa ulimwenguni wa umri wa kufanya kazi - unaochukuliwa kama umri wa miaka 15 au zaidi (milioni 245.6) - wafanyikazi wahamiaji husimamia asilimia 68.8.

Katika mwaka wa 2019, asilimia 67 ya wafanyikazi wahamiaji walikuwa wakiishi katika nchi zenye mapato ya juu - watu wanaokadiriwa kuwa milioni 113.9. Wafanyikazi wahamiaji milioni 49 (29%) zaidi walikuwa wakiishi katika nchi za mapato ya kati, na milioni 6.1 (3.6%) walikuwa katika nchi zenye mapato ya chini. Ingawa hatuwezi kulinganisha idadi ya wafanyikazi wahamiaji kwa kipindi cha muda mrefu, ni muhimu kuchunguza mabadiliko katika uwiano wa usambaaji. Mrundiko wa wafanyikazi wahamiaji wa kimataifa katika nchi zenye mapato ya juu-kati na mapato ya juu umesalia kuwa asilimia 86.4 katika mwaka wa 2013, asilimia 86.5 mnamo 2017 na asilimia 86.9 mnamo 2019. Hata hivyo, kulikuwa na mabadiliko dhahiri katika kategoria hizi mbili baada ya muda; yaani, kutoka 2013 hadi 2019, nchi za mapato ya juu zilizpata punguo la asilimia 7.3 ya wafanyikazi wahamiaji (kutoka 74.7% hadi 67.4%), huku nchi zenye mapato ya juu-kati zikipata ongezeko la asilimia 7.8 (kutoka 11.7% hadi 19.5%) (tazama Kielelezo cha 10). Mabadiliko haya dhahiri yanaweza kuathiriwa na ukuaji wa uchumi katika nchi za mapato ya kati na/au mabadiliko ya kanuni za uhamiaji wa wafanyikazi katika nchi zenye mapato ya juu. Mgao wa wafanyikazi wahamiaji katika jumla ya wafanyikazi wote katika vikundi vya mapato ya nchi ulikuwa mdogo sana katika nchi za mapato ya chini (2.3%) na katika nchi zenye mapato ya chini kiasi na juu-kati (1.4% na 2.2%, mtawalia), lakini mkubwa zaidi kwa nchi zenye mapato ya juu (18.2%).

Kielelezo cha 10. Wafanyikazi wahamiaji kulingana na kiwango cha mapato ya nchi, 2013, 2017 na 2019




*Chanzo*: ILO, 2018; ILO, 2021.

25 Yaliyomo katika kifungu hiki kidogo yamejikita na kutolewa kutoka ILO, 2021. Tafadhali rejelea hati hii kwa maelezo ya kiufafanuzi, uchanganuzi wa kina, udhaifu na tahadhari zinazohusiana na takwimu na mienendo iliyowasilishwa. Kwa ujumla zaidi, taarifa kuhusu ajira ya wazaliwa wa kigeni katika nchi za OECD inapatikana katika OECD, n.d.b.

26 Tazama, kwa mfano, ILO, 2021.

Wafanyakazi wahamiaji wanaume walikuwa wengi kuliko wafanyikazi wahamiaji wanawake kwa milioni 28.8 katika mwaka wa 2019, kukiwa na wanaume milioni 98.9 (58.5%) na wanawake milioni 70.1 (421.5%), katika hali ambayo wanaume walikuwa na idadi kubwa ya wahamiaji wa kimataifa wa umri wa kufanya kazi (milioni 128 au 52.1 %, ikilinganishwa na wanawake milioni 117.6 au 47.9%). Hali hii inawakilisha mabadiliko madogo tangu mwaka wa 2013, kuelekea kwenye idadi ya wafanyikazi wahamiaji wenye uwiano wa kijinsia, wakati mgao wa wafanyikazi wanaume ulikuwa asilimia 55.7 na wanawake asilimia 44.3. Tazama Jedwali la 2 kwa uainishaji zaidi wa kiwango cha mapato na jinsia.

### Jedwali la 2. Wafanyikazi wahamiaji wa kimataifa, kulingana na jinsia na kiwango cha mapato ya nchi wanayokwenda, 2019

| | Wafanyikazi wahamiaji (milioni) | | | Uwiano wa wafanyikazi wahamiaji wote (%) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **KIUME** | **KIKE** | Jumla | **KIUME** | **KIKE** | Jumla |
| Mapato ya chini | 3.7 | 2.4 | 6.1 | 2.2 | 1.4 | 3.6 |
| Mapato ya chini-kati | 10.5 | 5.6 | 16.0 | 6.2 | 3.3 | 9.5 |
| Mapato ya juu-kati | 19.5 | 13.5 | 33.0 | 11.5 | 8.0 | 19.5 |
| Mapato ya juu | 65.3 | 48.5 | 113.9 | 38.6 | 28.7 | 67.4 |
| **Jumla Duniani** | **98.9** | **70.1** | **169.0** | **58.5** | **41.5** | **100.0** |


*Chanzo*: ILO, 2021.

Kama inavyodhihirika katika data, idadi ya wafanyikazi wahamiaji wa kimataifa hivi sasa inaegemea jinsia moja na kijiografia wanapatikana mahali pamoja. Kuna idadi kubwa zaidi ya wafanyikazi wahamiaji wanaume ulimwenguni kuliko wanawake (tazama Jedwali la 2), kukiwa na muundo wa kijinsia ambao unabainisha idadi kubwa zaidi ya wanaume katika nchi zenye mapato ya chini na za mapato ya kati-chini ikilinganishwa na wanawake, na kinyume na mgawanyo wa kijinsia katika nchi zenye mapato ya juu.

Kijiografia, na kama inavyoonekana katika Kielelezo cha 11 hapa chini, milioni 102.4 au karibu asilimia 61 ya wahamiaji wote waliishi katika kanda ndogo tatu: Kaskazini mwa Marekani; Mataifa ya Kiarabu; na Kaskazini, Kusini na Magharibi mwa Ulaya.[27] Hasa, kuna ukosefu mkubwa wa urari wa kijinsia wa wafanyikazi wahamiaji katika kanda mbili: Kusini mwa Asia (wanaume milioni 5.7 ikilinganishwa na wanawake milioni 1.4) na Mataifa ya Kiarabu (wanaume milioni 19.9 ikilinganishwa na wanawake milioni 4.2). Ukanda wa Mataifa ya Kiarabu ni mojawapo ya sehemu kuu wanazokwenda wafanyikazi wahamiaji, ambapo wanajumuisha asilimia 41.4 ya wafanyikazi wote, aghalabu wakitawala sekta zote muhimu.

27 Kategoria ya ILO ya"Nchi za Kiarabu" inajumuisha nchi na maeneo yafuatayo: Bahrain, Iraki, Jordan, Kuwait, Lebanon, Oman, Qatar, Saudi Arabia, Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, Milki za Kiarabu, Yemen na Maeneo ya Palestina.

Kielelezo cha 11. Usambaaji wa kijiografia wa wafanyikazi wahamiaji kulingana na jinsia (milioni), 2019




*Chanzo*: ILO, 2021.

*Kumbuka*: Kielelezo hiki kinaonyesha kanda na sehemu za kijiografia za ILO, wala haimaanishi uidhinishaji au kukubalika rasmi na IOM. Tafadhali tazama Kiambatisho A cha ILO, 2021 kwa habari zaidi juu ya migawanyo ya kikanda. Tafadhali kumbuka kuwa sehemu iliyobakia ya sura hii inarejelea kanda za kijiografia za UN DESA.

## Programu za IOM za kusaidia kurejea nyumbani kwa hiari na ujumuishwaji upya

IOM inatekeleza mipango ya kusaidiwa kurejea nyumbani na kujumuishwa upya (AVRR) tangu mwaka wa 1979. Usaidizi wa AVRR ya IOM kwa wahamiaji unajumuisha shughuli mbalimbali na kwa kawaida hujumuisha: utoaji wa ushauri nasaha kabla ya kuondoka, ununuzi wa tiketi za ndege, usaidizi wa kiutawala na wa kusafiri na, ikiwezekana, utoaji wa usaidizi wa kujumuishwa tena katika jamii.

Kwa wastani, kutoka 2005 hadi 2014, IOM ilisaidia wahamiaji 34,000 kila mwaka kupitia AVRR. Kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha uhamiaji katika miaka ya hivi karibuni, idadi ya wanaorejea nayo imeongezeka (hadi kufikia wakati wa UVIKO-19). Katika mwaka wa 2019, msaada wa AVRR ulitolewa kwa wahamiaji 64,958 waliokuwa wanarudi kutoka nchi wenyeji au za mpito 136 wakisafiri kwenda nchi au maeneo ya asili 164 . Hata hivyo, idadi hii ilipungua katika mwaka wa 2020 kwa sababu ya UVIKO-19. Mwaka mzima wa 2020, usaidizi wa AVRR ulitolewa kwa wahamiaji 42,181 (15,149 katika Q1, 2,588 katika Q2, 10,521 katika Q3 na 13,923 katika Q4) waliokuwa wakirejea kutoka nchi wenyeji au za mpito au maeneo 139 (88 katika Q1, 41 katika Q2, 84 katika Q3 na 122 katika Q4) kwenda kwa nchi au maeneo ya asili 150 (136 katika Q1, 70 katika Q2, 110 katika Q3 na 132 katika Q4).

*Chanzo*: IOM, 2020d; IOM, 2020e; IOM, 2002f.

## Utumaji wa pesa kimataifa

Utumaji wa pesa ni uhamishaji wa pesa au bidhaa unaofanywa na wahamiaji moja kwa moja hadi kwa familia au jamii katika nchi zao za asili. Benki ya Dunia hukusanya data za kimataifa juu ya utumaji wa pesa kimataifa, licha ya upungufu mwingi wa data, tofauti za kiufafanuzi na changamoto za mbinu katika kukusanya takwimu sahihi.[28] Hata hivyo, data zake, hazinasi mtiririko usiorekodiwa kupitia njia rasmi au zisizo rasmi, na kwa hivyo ukubwa halisi wa utumaji wa pesa au bidhaa ulimwenguni unaweza kuwa mkubwa kuliko makadirio yanayotolewa.[29] Suala hili limejitokeza wakati wa ugonjwa huu tandavu, kufuatia matokeo chanya zaidi katika mwaka wa 2020 kwa mtiririko wa pesa zilizotumwa kimataifa, kinyume na makadirio ya awali yasiyotia moyo; hii ilitokana kwa kiasi na kuhama kutoka kwa njia zisizo rasmi hadi kwa njia rasmi ili kukabiliana na vikwazo vya usafiri vya UVIKO-19, miongoni mwa sababu zingine (tazama kisandiku cha maandishi hapo chini).[30] Licha ya masuala hayo, data zilizopo zinaonyesha mwenendo wa ongezeko la muda mrefu la utumaji pesa kimataifa katika miaka ya hivi karibuni, ikiongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 128 katika mwaka wa 2000 hadi Dola za Marekani bilioni 702 katika mwaka wa 2020.

Licha ya makadirio ya awali ya kushuka kwa asilimia 20 kwa pesa zinazotumwa kimataifa duniani kote katika mwaka wa 2020 (yaliyofanywa Aprili ya mwaka huo),[31] data ya kila mwaka inaonyesha kuwa kulikuwa na upunguaji mdogo wa kutuma fedha duniani (punguo la 2.4%) katika mwaka wa 2020, uliofikia Dola za Marekani bilioni 702, zikiwa zimepungua kutoka Dola za Marekani bilioni 719 katika mwaka wa 2019. Hata hivyo, miaka yote mitatu mfululizo kabla ya 2020 ilishuhudia ongezeko: kutoka 2016 hadi 2019, mtiririko wa pesa zilizotumwa (ndani) duniani uliongezeka kwa wastani wa asilimia 7.2, kutoka Dola za Marekani bilioni 597 mnamo 2016 hadi bilioni 640 mnamo 2017, na kwa asilimia 8.4 na asilimia 3.6 kutoka 2017 hadi 2018 (kutoka Dola za Marekani bilioni 640 hadi bilioni 694) na kutoka 2018 hadi 2019 (kutoka Dola za Marekani bilioni 694 hadi bilioni 719), mtawalia. Zikifuata mtindo huu, pesa zilizotumwa kwa nchi za mapato ya chini na kati (ambazo zinachukua idadi kubwa ya jumla yote duniani) zilipungua katika mwaka wa 2020 (kutoka Dola bilioni 548 katika mwaka wa 2019 hadi bilioni 540) baada ya mwenendo chanya kutoka 2016 hadi 2018 (kutoka Dola za Marekani bilioni 441 katika mwaka wa 2016 hadi bilioni 478 katika mwaka wa 2017 na Dola za marekani bilioni 524 mnamo 2018). Tangu katikati ya miaka ya 1990, pesa zilizotumwa kimataifa zimezidi kwa kiasi kikubwa viwango rasmi vya usaidizi wa maendeleo vinavyofafanuliwa kama misaada ya serikali iliyotayarishwa kukuza maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa nchi zinazoendelea (tazama Kielelezo cha 12 hapo chini).[32]

28 Yaliyomo katika sehemu kubwa ya kifungu hiki, isipokuwa kama imebainishwa vinginevyo, yamejikita na kutolewa kutoka data ya Benki ya Dunia inayohusu uhamiaji na utumaji pesa (Benki ya Dunia, n.d.). Hasa, seti za data za kila mwaka za Benki ya Dunia (ibid.), *Migration and Development Brief 34* (Ratha et al., 2021), na taarifa yake kwa vyombo vya habari ya tarehe 12 Mei (World Bank, 2021a) ni vyanzo muhimu vya habari. Tafadhali rejelea vyanzo hivi na pia vile vya Benki ya Dunia *Factbooks on Migration and Development*, kikiwemo kile cha hivi punde zaidi, kilichochapishwa katika mwaka wa 2016, kwa maelezo ya kiufafanuzi, uchanganuzi wa kina, tahadhari, udhaifu na mbinu zinazohusishwa na takwimu na mienendo iliyowasilishwa.


29 World Bank, 2016.

30 IMF, 2020; IOM, 2020g; IOM, 2020h; IOM, 2020i; IOM, 2021b.

31 Ratha et al., 2020a.

32 Tazama, kwa mfano, OECD, n.d.c, ambayo pia inazo data za usaidizi rasmi wa maendeleo. Kuna kundi kubwa la machapisho yanayozidi kuongezeka yanayochunguza athari za kimaendeleo, kiuchumi na kijamii za mwenendo huu.

Kielelezo cha 12. Mtiririko wa fedha zilizotumwa kimataifa hadi kwa nchi zenye mapato ya chini na kati (1990–2020)




*Chanzo*: World Bank, n.d. (ilisomwa Juni 2021).
*Kumbuka:* Namba zote ziko katika blioni za Dola za Marekani za sasa (thamani bayana).

Mnamo 2020, Uchina, Meksiko, Ufilipino na Misri zilikuwa (kwa mpangilio wa kutoka juu kuja chini) nchi tano kuu zinazopokea pesa zilizotumwa, ingawa India na Uchina zilikuwa juu zaidi ya nchi zingine, huku jumla ya pesa zilizotumwa kuja katika nchi hizo zikizidi Dola za Marekani bilioni 59 kwa kila nchi (tazama Jedwali la 3). Nchi za G7 Ufaransa na Ujerumani zilisalia katika nchi 10 kuu zinazopokea mapato duniani kote katika mwaka wa 2020, kama ilivyokuwa tangu mwaka wa 2005 (tazama Jedwali la 3). Hata hivyo, ikumbukwe kwamba nyingi za pesa zilizoingia si za matumizi ya nyumbani, bali zinahusiana na mishahara ya wafanyikazi wanaovuka mipaka ambao wanafanya kazi Uswisi huku wakiishi Ufaransa au Ujerumani.[33]

33 Eurostat, 2020.


Jedwali la 3. Nchi 10 zinazoongoza katika kupokea/kutuma pesa kimataifa (2005–2020) (bilioni za Dola za Marekani sasa)

| Nchi zinazopokea pesa nyingi zilizotumwa | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2005 | | 2010 | | 2015 | | 2020 | |
| Uchina | 23.63 | India | 53.48 | India | 68.91 | India | 83.15 |
| Meksiko | 22.74 | Uchina | 52.46 | Uchina | 63.94 | Uchina | 59.51 |
| India | 22.13 | Meksiko | 22.08 | Ufilipino | 29.80 | Meksiko | 42.88 |
| Nigeria | 14.64 | Ufilipino | 21.56 | Meksiko | 26.23 | Ufilipino | 34.91 |
| Ufaransa | 14.21 | Ufaransa | 19.90 | Ufaransa | 24.07 | Misri | 29.60 |
| Ufilipino | 13.73 | Nigeria | 19.74 | Nigeria | 20.63 | Pakistani | 26.11 |
| Ubelgiji | 6.88 | Ujerumani | 12.79 | Pakistani | 19.31 | Ufaransa | 24.48 |
| Ujerumani | 6.86 | Misri | 12.45 | Misri | 18.33 | Bangladeshi | 21.75 |
| Uhispania | 6.66 | Ubelgiji | 10.99 | Ujerumani | 15.58 | Ujerumani | 17.90 |
| Poland | 6.47 | Bangladeshi | 10.85 | Bangladeshi | 15.30 | Nigeria | 17.21 |
| **Nchi zinazotuma pesa nyingi nje** | | | | | | | |
| 2005 | | 2010 | | 2015 | | 2020 | |
| Marekani | 47.75 | Marekani | 50.53 | Marekani | 60.72 | Marekani | 68.00 |
| Saudi Arabia | 14.30 | Saudi Arabia | 27.07 | Milki za Kiarabu | 40.70 | Milki za Kiarabu | 43.24 |
| Ujerumani | 12.71 | Shirikisho la Urusi | 21.45 | Saudi Arabia | 38.79 | Saudi Arabia | 34.60 |
| Uswisi | 10.86 | Uswisi | 18.51 | Uswisi | 26.03 | Uswisi | 27.96 |
| Uingereza | 9.64 | Ujerumani | 14.68 | Shirikisho la Urusi | 19.69 | Ujerumani | 22.02 |
| Ufaransa | 9.47 | Italia | 12.88 | Ujerumani | 18.25 | Uchina | 18.12 |
| Jamhuri ya Korea | 6.90 | Ufaransa | 12.03 | Kuwait | 15.20 | Shirikisho la Urusi | 16.89 |
| Shirikisho la Urusi | 6.83 | Kuwait | 11.86 | France | 12.79 | France | 15.04 |
| Luxembourg | 6.74 | Luxembourg | 10.66 | Qatar | 12.19 | Luxembourg | 14.20 |
| Malaysia | 5.68 | Milki za Kiarabu | 10.57 | Luxembourg | 11.19 | Uholanzi | 13.92 |

*Chanzo*: World Bank, n.d. (ilisomwa Juni 2021).
*Kumbuka*: Namba zote ziko katika blioni za Dola za Marekani za sasa (thamani bayana).

Hakuna maafikiano kuhusu jinsi “kutegemea kupita kiasi” utumaji pesa kimataifa kunavyoweza kufafanuliwa, lakini utegemezi wa pesa zilizotumwa kutoka nje hupimwa zaidi kama uwiano wa pesa zinazotumwa na pato ghafi la ndani (GDP). Hivi sasa kuna nchi 29 (kati ya nchi 177 zilizoripotiwa) ambazo zina uwiano wa pesa zinazotumwa na zao ghafi la ndani wa zaidi ya asilimia 10. Nchi tano zilizoongoza katika kupokea pesa zilizotumwa ukilinganisha na mgao wa pato ghafi la ndani katika mwaka wa 2020 zilikuwa Tonga (37.7%), ikifuatwa na Somalia (35.3%), Lebanon (32.9%), Sudan Kusini (29.5%) na Kirigizstani (29.4%). Huku nchi nyingi zikidumisha viwango vilevile katika mwaka wa 2020 kama ilivyokuwa katika mwaka wa 2019, mgao wa pato ghafi la ndani nchini Lebanon uliongezeka mara tatu wakati pato ghafi la ndani likiporomoka katika mwaka wa 2020. Kinyume chake ni kuwa uchumi wa Haiti wa utumaji fedha kama mgao wa pato ghafi la ndani ulipungua kwa nusu kwa sababu ya upatikanaji mdogo wa sarafu za nchi na uwezekano wa kupanda kwa gharama za kutuma. Kutegemea sana pesa zinazotumwa kunaweza kukuza utamaduni wa utegemezi katika nchi inayopokea, na hivyo basi kupunguza ushiriki wa nguvukazi na kupunguza kasi ya ukuaji wa kiuchumi.[34] Utegemezi mwingi wa pesa zilizotumwa pia huufanya uchumi kuwa mwepesi wa kuathiriwa na mabadiliko ya ghafla katika pesa zinazopokelwa.[35]

Kielelezo cha 13. Nchi/maeneo 20 ya wapokeaji wakuu wa fedha zinazotumwa kwa jumla ya bilioni za USD (kushoto) na mgao wa GDP (kulia), 2019–2020





*Chanzo*: World Bank, n.d. (ilisomwwa Juni 2021).
*Kumbuka:* Namba zote ziko katika blioni za Dola za Marekani za sasa (thamani bayana). Yemen haijajumuishwa kwa kuwa data ya utumwaji pesa haijasasishwa.

34 Amuedo-Dorantes, 2014.
35 Ghosh, 2006.

Karibu kila wakati nchi zenye mapato ya juu ndizo chanzo kikuu cha pesa zinazotumwa kimataifa. Kwa miongo kadhaa, Marekani imekuwa nchi inayoongoza katika utumaji wa pesa duniani, ikiwa ilituma nje Dola za Marekani bilioni 68 mnamo 2020, ikifuatwa na Milki za Kiarabu (Dola za Marekani bilioni 43.24), Saudi Arabia (Dola za Marekani bilioni 34.60) na Uswisi (Dola za Marekani bilioni 27.96). Nchi ya tano iliyotuma nje pesa nyingi katika miaka ya 2019 na 2020 ni Ujerumani (ikiwa na mtiririko nje wa Dola za Marekani bilioni 23.94 na bilioni 22.02 mtawalia). Mbali na jukumu lake kama mpokeaji mkuu, Uchina (iliyoainishwa kama nchi ya mapato ya kati na Benki ya Dunia) pia imekuwa chanzo kikubwa cha fedha zinazotumwa kimataifa, ikituma Dola za Marekani bilioni 15.14 katika mwaka wa 2019 na Dola za Marekani bilioni 18.12 ziliripotiwa katika mwaka wa 2020.

Kielelezo cha 14. Nchi 20 zinazoongoza katika utumaji pesa kimataifa kwa jumla katika bilioni za Dola za Marekani (kushoto) na mgao wa GDP (kulia), 2019–2020




*Chanzo*: World Bank, n.d. (ilisomwa Juni 2021)
*Maelezo:* Namba zote ziko katika blioni za Dola za Marekani za sasa (thamani bayana).

## UVIKO-19, utumaji pesa kimataifa na udigitishaji

Mnamo 2020, wachanganuzi wengi uliwenguni walikuwa wakifuatilia kwa karibu taarifa na uchanganuzi wa hivi punde ili kuelewa athari za uhamiaji na usafiri za UVIKO-19 kwa utumaji wa pesa kimataifa.[a] Katika mwaka wote wa 2020, data ya utumaji pesa kutoka nchi kadhaa ilikiuka makadirio ya Benki ya Dunia ya kupungua kwa kiasi kikubwa cha pesa zinazotumwa duniani kote, huku baadhi ya nchi zikivunja rekodi ya pesa zinazoingia kila mwezi baada ya nusu ya kwanza ya mwaka 2020.

Kulingana na ripoti ya Benki ya Dunia ya Mei 2021,[b] mtiririko wa utumaji pesa umeimarika wakati wa tatizo la UVIKO-19. Mnano 2020, mtiririko rasmi uliorekodiwa wa pesa zilizotumwa ulifika Dola za Marekani bilioni 702, asilimia 2.4 tu chini ya Dola za Marekani bilioni 719 zilizoonekana katika mwaka wa 2019, jambo ambalo ni kinyume kabisa na makadirio ya hapo awali (Dola za Marekani bilioni 572 mnamo Aprili 2020[c] na Dola za Marekani bilioni 666 mnamo Oktoba 2020[d]).

Pamoja na uwekaji wa sera ili kusaidia utumaji pesa na hali bora za kiuchumi, kuziacha njia zisizo rasmi (k.m. kuvuka mipaka ukiwa umebeba pesa) na kuelekea kwa njia rasmi zaidi kupitia kwa ongezeko la udiijitishaji wa uhawilishaji fedha kulionekana kuwa moja ya mambo muhimu zaidi katika kueleza mwendo wa polepole wa mtiririko wa utumaji pesa kudorora kinyume na makadrio. Kwa hiyo, kuna uwezekano wa data rasmi kunasa utumaji pesa mwingi hata kama huenda ukubwa halisi wa jumla ya pesa zilizotumwa kimataifa (rasmi na zisizo rasmi) umeshuka. Kwa mfano, nchini Meksiko, mtiririko wa utumaji pesa ulibadilika kutoka hali isiyo rasmi hadi iliyo rasmi kwa kuwa vivuko vya mpakani vilifungwa katika mwaka wa 2020 na uhawilishaji fedha kielektroniki ukawa chaguo la pekee la kutuma pesa.[e]

Nchi kadhaa zimechukua hatua za kuhimiza matumizi ya huduma za kidijiti wakati wa ugonjwa huu tandavu, na majukwaa ya pesa ya rununu yamefanya uhawilishaji wa pesa kuwa wa bei nafuu na wa haraka kuliko matumizi ya pesa taslimu na uhawilishaji wa benki. Kupitia pesa za rununu, utumaji pesa umekuwa rahisi kufuatiliwa, na kuifanya njia hii kuwa salama zaidi kuliko njia zisizo rasmi.[f]

Hata hivyo, gharama ya kutuma pesa nyumbani, hasa katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, bado ni za juu licha ya juhudi za kimataifa za kupunguza gharama za utumaji pesa kimataifa tangu mwishoni mwa miaka ya 2000. Kufikia Machi 2021, kutuma pesa duniani kunagharimu wastani wa asilimia 6.38 ya kiasi kilichotumwa (Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa yanalenga kuipunguza hadi chini ya 3%) na asilimia 26 ya njia za nchi hadi nchi ni zaidi ya gharama jumla ya asilimia 5 (Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa yanalenga kufikia sifuri kwenye njia kama hizo).[g]

UVIKO-19 inaweza kutoa msukumo wa ziada wa kutumia teknolojia ili kupanua zaidi njia za utumaji pesa na kupunguza gharama.

a IOM, 2020g; IOM, 2020h; IOM, 2020i, IOM, 2021b.
b Ratha et al., 2021.
c Ratha et al., 2020a.
d Ratha et al., 2020b.
e Dinarte et al., 2021.
f Aron na Muellbauer, 2019.
g World Bank, 2021b.

## Wakimbizi na waomba hifadhi

Kufikia mwisho wa 2020, kulikuwa na jumla ya wakimbizi milioni 26.4 ulimwenguni, huku milioni 20.7 wakiwa chini ya mamlaka ya UNHCR na wakimbizi milioni 5.7 wakiwa wamesajiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Usaidizi na Kazi (UNRWA) kwa Wakimbizi wa Palestina walio Mashariki ya Kati.[36] Idadi jumla hii ya wakimbizi ndiyo ya juu zaidi kurekodiwa, ingawa kiwango cha ukuaji wa kila mwaka kimepungua tangu 2012.

Pia kulikuwa na takribani watu milioni 4.1 wanaotafuta ulinzi wa kimataifa huku wakisubiri uamuzi wa hali yao ya ukimbizi, wanaojulikana kama waomba hifadhi. Mnamo 2020, idadi ya madai ya kwanza ya kuomba hifadhi yaliyowasilishwa duniani yalikuwa milioni 1.1. Kushuka huku kwa asilimia 45 kutoka milioni 2 ya mwaka uliopita kunawakilisha punguo moja kubwa zaidi tangu mwaka wa 2000, wakati maombi ya hifadhi yalipoanza kujumlishwa duniani kote na UNHCR, na hii ilikuwa ni matokeo ya moja kwa moja ya vikwazo vya usafiri vilivyotokana na UVIKO-19. Mpokeaji mkuu alibaki kuwa Marekani na takribani madai 250,000, punguo la asilimia 14 kutoka mwaka uliotangulia (301,000). Iliyoshika nafasi ya pili ilikuwa Ujerumani, ikiwa na madai mapya 102,600, likiwa punguo kubwa kutoka mwaka wa 2019 (142,500), na ya chini zaidi kurekodiwa katika takribani miaka 10.

Mwishoni mwa 2020, wale walio chini ya umri wa miaka 18 walikuwa karibu asiimia 38 ya idadi ya wakimbizi (wakimbizi milioni 8 kati ya milioni 20.7 walio chini ya mamlaka ya UNHCR). Watoto wasio na walezi na waliotenganishwa (UASC) walituma takribani maombi ya kibinafsi 21,000 ya hifadhi katika mwaka wa 2020, ambayo yalipungua kutoka 25,000 katika mwaka uliotangulia.

Kama ilivyoelezwa katika ripoti za awali, mienendo ya migogoro ambayo haijatatuliwa au inayoibuka upya katika nchi muhimu ilichangia pakubwa kupatikana kwa takwimu na mienendo ya sasa. Kuhusu wakimbizi walio chini ya mamlaka ya UNHCR kufikia mwishoni mwa 2020, nchi 10 kuu wanakotoka wakimbizi wengi – Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, Afghanistani, Sudan Kusini, Myanmar, Jamhuri ya Kiarabu ya Congo, Somalia, Sudan, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Eritrea na Burundi – zilichangia zaidi ya asilimia 80 ya jumla ya idadi ya wakimbizi. Nyingi za nchi hizi zimekuwa miongoni mwa chimbuko kuu la wakimbizi kwa angalau miaka saba iliyopita.


Mzozo ambao umeendelea kwa muongo mzima katika Jmahuri ya Kiarabu ya Syria ulishuhudia idadi ya wakimbizi kutoka nchi hiyo wakifika takribani milioni 6.7. Hili lilikuwa ni ongezeko la takriban 100,000 kutoka mwaka uliopita na kufikia mwaka wa saba mfululizo kama taifa kuu la asili ya wakimbizi. Ukosefu wa utulivu na ghasia ambazo zimeifanya Afghanistani kuwa chanzo kikuu cha wakimbizi kwa zaidi ya miaka 30 vimeendelea, huku nchi hiyo ikiwa ya pili kama chanzo cha wakimbizi wengi zaidi duniani, ikiwa na wakimbizi milioni 2.6 katika mwaka wa 2020; idadi hii imepungua ukilinganisha na takwimu za 2019 (milioni 2.7). Sudan Kusini imesalia kuwa nchi ya tatu ya asili ya wakimbizi wengi tangu vurugu zilipozuka katikati mwa 2016, ikiwa na wakimbizi milioni 2.2 kufikia mwishoni mwa 2020. Wakimbizi kutoka Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, Afghanistani, Sudan Kusini, Myanmar na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo walijumuisha zaidi ya nusu ya idadi ya wakimbizi duniani. Kielelezo cha 15 kinaonyesha mwenendo wa idadi ya wakimbizi katika nchi tano kuu zilizo asili ya wakimbizi kuanzia 2005 hadi 2020. Athari za vita vya Syria inaonekana wazi; katika mwaka wa 2010, Jamhuri ya Kiarabu ya Syria ilikuwa nchi asili ya wakimbizi na waomba hifadhi wanaopungua 30,000, ilhali ilikuwa nchi mwenyeji wa wakimbizi ya tatu kwa wingi wao duniani, ikiwa na zaidi ya wakimbizi milioni 1 hasa wakitokea Iraki.[37]

---

36 Yaliyomo katika kifungu hiki yamejikita na kutolewa kutoka UNHCR, 2021a. Tafadhali rejelea hati hizi kwa maelezo ya kiufafanuzi, uchanganuzi wa kina, tahadhari, vikwazo na mbinu zinazohusiana na namba na mienendo iliyowasilishwa. Ripoti za awali za Mienendo ya Dunia, pamoja na hifadhidata yake ya Takwimu za Idadi ya Watu (UNHCR, n.d.a) ni vyanzo vingine muhimu vya habari.

37 UNHCR, 2011.


Kielelezo cha 15. Idadi ya wakimbizi wa nchi 5 kuu za asili, 2005–2020 (milioni)




*Chanzo*: UNHCR, n.d.a. (ilisomwa 23 Juni 2021).
*Kumbuka*: Sudan Kusini ilikuwa nchi mnamo 2011.

Kama ilivyokuwa katika miaka iliyopita, zaidi ya nusu ya wakimbizi wote waliishi katika nchi 10. Katika mwaka wa 2020, kwa mwaka wa tano mfululizo, Uturuki ilikuwa nchi kubwa zaidi mwenyeji duniani, ikiwa na zaidi ya wakimbizi milioni 3.6, hasa kutoka Syria. Ikidhihirisha sehemu kubwa ya Wasyria katika idadi ya wakimbizi duniani, nchi inayopakana nayo ya Lebanon pia ilikuwa miongoni mwa nchi 10 kuu zilizo wenyeji wa wakimbizi wengi. Pakistani na Jamhuri ya Kiislamu ya Iran zilikuwa pia miongoni mwa nchi 10 kuu zinazohifadhi wakimbizi, kama nchi mbili kuu zinazohifadhi wakimbizi kutoka Afghanistani, nchi asili ya wakimbizi ya pili. Nchi hizo zingine zilijumuisha Uganda, Ujerumani, Sudan, Bangladeshi na Ethiopia. Idadi kubwa (73%) ya wakimbizi walifadhiliwa katika nchi jirani. Kwa mujibu wa UNHCR, nchi zenye maendeleo duni zaidi – kama vile Bangladeshi, Chad, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Ethiopia, Rwanda, Sudan Kusini, Sudan, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Uganda na Yemen – zilikuwa wenyeji wa asilimia 27 ya jumla ya wakimbizi ulimwenguni (wakimbizi milioni 6.7).

Kielelezo cha 16. Idadi ya wakimbizi katika nchi 5 kuu zinazowahifadhi kufikia 2020 (milioni)




*Chanzo*: UNHCR, n.d.a (ilisomwa 23 Juni 2021).


Mnanmo 2020, zaidi ya wakimbizi 250,000 walirudi katika nchi zao za asili, punguo la asilimia 21 kuliko ilivyokuwa katika mwaka uliotangulia (317,000). Karibu nusu (122,000) ya waliorejea walienda Sudan Kusini, wengi wao wakitoka Uganda (74,000). Katika mwaka wa 2020, Sudan Kusini iliipiku Jamhuri ya Kiarabu ya Syria kwa kuwa na wakimbizi wengi waliorejea.

Ingawa kuna changamoto nyingi za kupima wale wanaofaidika na ujumuishaji wa ndani, UNHCR inakadiria kuwa, mnamo 2020, nchi 28 ziliripoti anagalau mkimbizi mmoja aliyepata uraia wa kuandikishwa (ikilinganishwa na nchi 25 katika mwaka wa 2019), kukiwa na jumla ya wakimbizi 34,000 waliopata uraia wa kujiandikisha katika mwaka huo – wakiwa wamepungua kabisa kutoka wakimbizi wapya 55,000 waliopata uraia wa kujiandikisha katika mwaka wa 2019, lakini bado likiwa ongezeko kubwa ikilinganishwa na 23,000 walioripotiwa katika mwaka wa 2016. Katika mwaka wa 2020, asilimia 85 ya uraia wa kuandikishwa ulifanyika Ulaya, wengi wao (takriban wakimbizi 25,700) wakiwa Uholanzi. Nchi zilizokuwa katika nafasi za pili na tatu zilikuwa Canada (takribani 5,000) na Ufaransa (takribani 2,500).

Mnamo 2020, takribani wakimbizi 34,400 walipokelewa na kupewa makazi mapya duniani kote, ikiwasilisha upunguaji mkubwa kutoka mwaka wa 2019, ambapo wakimbizi zaidi ya 107,700 walipewa makazi mapya. Nchi kuu zilizotoa makazi mapya zilikuwa Marekani na Canada, zikiwa na takribani wakimbizi 9,600 na 9,200 mtawalia, na huu ulikuwa upunguaji mkubwa kutoka mwaka uliotangulia ambapo kulikuwa na 27,500 (Marekani) na 30,100 (Canada). Umoja wa Ulaya ulitoa makazi mapya kwa jumla ya wakimbizi 11,600. Wasyria ndio walionufaika zaidi, wakiwa theluthi moja ya wakimbizi waliopewa makazi mapya, wakifuatwa na Wakongo (12%).

Upunguaji mkubwa wa utoaji wa makazi mapya kwa wakimbizi unaweza kuelezwa kwa kiasi kidogo kuwa ni athari za ugonjwa tandavu, ambao ulipunguza sana safari za kimataifa duniani kote. Sababu nyingine ya kupungua kwa idadi ya wakimbizi waliopewa makazi mapya nchini Marekani ilitokana na kupunguzwa kikomo cha juu cha wakimbizi wanaoruhusiwa (idadi ya wakimbizi wanaokubaliwa kupewa makazi mapya kila mwaka wa fedha) na kuimarishwa kwa ukaguzi wa kiusalama kwa wakimbizi wanaotoka kwenye nchi za "hatari-kubwa", ambayo imekuwa na athari ya kupunguza idadi ya wakimbizi kutoka nchi hizo. Kielelezo cha 17 kinatoa muhtasari wa takwimu za makazi mapya kwa nchi muhimu kuanzia 2005 hadi 2020.

Kieleelzo cha 17. Idadi ya wakimbizi waliopewa makazi mapya na nchi zinazoongoza katika utoaji wa makazi mapya mnamo 2005–2020




*Chanzo*: UNHCR, n.d.b (ilisomwa 23 Juni 2021).

Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, idadi ya wakimbizi wanaohitaji makazi mapya imeongezeka sana, ikiwa karibu maradufu. UNHCR ilikadiria kwamba katika mwaka wa 2011 kulikuwa na takribani wakimbizi 805,000 waliohitaji kupewa makazi mapya, ambao wameongezeka na kufikia milioni 1.4 katika mwaka wa 2021.[38]

Idadi ya wakimbizi waliopewa makazi mapya imebadilikabadilika jinsi miaka ilivyosonga. Katika mwaka wa 2005, karibu wakimbizi 81,000 walipewa makazi mapya, ikilinganishwa na kama 34,000 katika mwaka wa 2020. Hata hivyo, katika mwaka wa 2019 idadi ya waliopewa makazi mapya ilikuwa karibu 108,000. Kwa jumla, utoaji wa makazi mapya haujaendana na ongezeko kubwa la mahitaji (tazama Jedwali la 4).

## Jedwali la 4. Idadi ya wakimbizi wanaohitaji makazi mapya na idadi ya wakimbizi waliopewa makazi mapya duniani kote, kuanzia 2005

| | Jumla ya makadirio ya mahitaji ya makazi mapya (pamoja na mipango ya miaka mingi), watu | Wanaofika kupewa makazi mapya |
|---|---|---|
| 2005 | – | 80 734 |
| 2006 | – | 71 660 |
| 2007 | – | 75 271 |
| 2008 | – | 88 772 |
| 2009 | – | 112 455 |
| 2010 | – | 98 719 |
| 2011 | 805 535 | 79 727 |
| 2012 | 781 299 | 88 918 |
| 2013 | 859 305 | 98 359 |
| 2014 | 690 915 | 105 148 |
| 2015 | 958 429 | 106 997 |
| 2016 | 1 153 296 | 172 797 |
| 2017 | 1 190 519 | 102 709 |
| 2018 | 1 195 349 | 92 348 |
| 2019 | 1 428 011 | 107 729 |
| 2020 | 1 440 408 | 34 383 |
| 2021 | 1 445 383 | – |

*Chanzo:* UNHCR, n.d.b (ilisomwa 23 Juni 2021).
*Maelezo:* *Ripoti ya Makadirio ya Mahitaji ya Makazi Mapya Duniani* iliyotayarishwa na UNHCR inapatikana kuanzia 2011.

38 UNHCR, 2021b.

## Jukumu la IOM katika utoaji wa makazi mapya

IOM hutekeleza jukumu muhimu katika utoaji wa makazi mapya duniani. Utoaji wa usaidizi muhimu kwa Mataifa katika kuwapa makazi wakimbizi na washiriki wengine wa misaada ya kibinadamu ni madhumuni ya kimsingi na ni miongoni mwa shughuli zake kubwa zinazoendelea. Mbali na programu za jadi za utoaji wa makazi mapya na kuhamisha makundi ya wakimbizi hadi nchi salama kwa sababu za kibinadamu, Mataifa mengi yanavutiwa au kwa sasa yanafanya aina zingine za ukubalifu, kama ufadhili wa kibinafsi, udhamini wa masomo na mipango ya kusafirisha wafanyikazi. Data za safari za IOM za usaidizi wa utoaji wa makazi mapya zinarejelea idadi jumla ya wakimbizi na watu wengine wahusika wanaosafiri chini ya ufadhili wa IOM kutoka nchi mbalimbali walikoondoka kwenda maeneo mengine duniani kote katika kipindi fulani.

Mnamo 2019, karibu watu 107,000 walisafiri chini ya ufadhili wa IOM kupitia programu za utoaji wa makazi mapya, kukiwa na shughuli muhimu kutoka Afghanistani, Misri, Ethiopia, Iraki, Jordan, Kenya, Lebanon, Uturuki, Uganda, Ukraine na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.[a] Kuhusu takwimu zilizotajwa hapo juu, karibu watu 30,000 waliohitaji ulinzi wa kimataifa walipewa makazi mapya katika nchi 18 tofauti za Ulaya, wakiwakilisha asilimia 30 ya idadi ya wanaohitaji kupewa makazi mapya na usaidizi wa kibinadamu unaotolewa na IOM.

Katika mwaka wa 2020, IOM ilisaidia zaidi ya Mataifa 27 kutoa makazi mapya, kuwapa wakimbizi hifadhi ya muda katika nchi za ulimwengu wa tatu na kuwahamisha hadi mahali pengine jumla ya wakimbizi 40,536 na watu wengine walio katika mazingira magumu, kukiwa na shughuli muhimu kutoka Afghanistani, Ugiriki, Jordan, Lebanon na Uturuki. Nchi tatu zilizoongoza katika utoaji wa makazi mapya zilikuwa Marekani, Canada na Uswidi. Kutokana na jumla iliyotajwa hapo juu, wanufaika 3.063 waliohitaji ulinzi wa kimataifa walihamishwa kutoka Ugiriki, Italia na Malta hadi nchi 14 katika Eneo la Kiuchumi la Ulaya, wengi wao wakisafirishwa kwa ndege za kukodi.

IOM huunga mkono Nchi Wanachama wake katika kutekeleza aina mbalimbali za makzi mapya, kuhamisha na mipango mingine ya kuwahifadhi wakimbizi katika nchi za ulimwengu wa tatu kwa muda, mingi ikiwa ni mipango iliyoanzishwa vyema, huku mingine ikiwa ni miitikio ya dharura kwa majanga mahususi ya uhamiaji wa kulazimishwa.

Kwa kuzingatia mahitaji makubwa na ukosefu wa maeneo yatakayotumika kwa makazi mapya, IOM inaendelea kuzungumza na wahusika kuhusu kuongeza upatikanaji wa njia salama na za kisheria. Chini ya mikataba ya ushirikiano, IOM huwapa wadau taarifa muhimu na hushiriki data na washirika wakuu, kama vile UNHCR, nchi zinazotoa makazi mapya na mashirika ya makazi. IOM inafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na UNHCR mara kwa mara ili kuthibitisha na kupanga vyema data ya jumla inayohusiana na utoaji wa makazi mapya, hasa kuhusu takwimu za wanaoondoka. Kwa taarifa zaidi kuhusu shughuli za makazi mapya za IOM, tazama www.iom.int/resettlement-assistance.

a IOM, 2020j.

## Wakimbizi wa ndani ya nchi

Kituo cha Ufuatiliaji wa Ufurushwaji wa Ndani (IDMC) hukusanya data juu ya aina mbili za ufurushwaji wa ndani: ufurushaji mpya wakati wa kipindi fulani, na jumla ya idadi ya IDP mahali fulani kila wakati. Habari hii ya kitakwimu imegawanywa na visababishi viwili vikuu vya ufurushwaji: (a) majanga, na (b) migogoro na vurugu. Hata hivyo, IDMC inakiri kuwepo kwa changamoto zinazohusiana na kutofautisha kati ya majanga na migogoro kama sababu ya mara moja ya ufurushwaji, na inaangazia mahitaji yanayoongezeka ya kutambua njia bora za kuripoti juu ya ufurushwaji katika muktadha wa vichocheo anuwai..[39] Hatua za kuzuia maenezi ya UVIKO-19 zimekwamisha ukusanyaji wa data ya watu waliofurushwa.[40]

Kwa makadirio ya milioni 48, jumla ya idadi ya watu walio wakimbizi wa ndani waliofurushwa na migogoro na vurugu katika nchi na maeneo 59 kufikia tarehe 31 Desemba 2020 ilikuwa ya juu zaidi kurekodiwa tangu IDMC ilipoanza ufuatiliaji katika mwaka wa 1998, na inawakilisha ongezeko kutoka kwa milioni 45.9 iliyoripotiwa mnamo 2019. Kama ilivyo kwa mienendo ya wakimbizi (ilijadiliwa katika sehemu iliyotangulia), migogoro mipya na isiyoweza kudhibitiwa kwa urahisi ilimaanisha kwamba idadi ya wakimbizi wa ndani waliofurushwa na migogoro na vurugu imekuwa karibu maradufu tangu mwaka 2000, na imeongezeka sana tangu mwaka 2010.

Kielelezo cha 18 kinaonyesha nchi 20 zinazoongoza ulimwenguni kwa kuwa na idadi kubwa zaidi ya IDP waliofurushwa kutoka kwa makazi yao kwa sababu ya vita na vurugu (idadi) mwishoni mwa 2020. Nchi nyingi zilikuwa katika Mashariki ya Kati au Afrika iliyo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Jamhuri ya Kiarabu ya Syria ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu waliokimbia makazi yao kwa sababu ya vita (milioni 6.6) kufikia mwisho wa 2020, ikifuatiwa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (milioni 5.3). Colombia ilikuwa ya tatu kwa idadi kubwa zaidi ikiwa na milioni 4.9, ikifuatwa na Yemen (milioni 3.6) na Afghanistani (milioni 3.5). Zaidi ya milioni 35 (karibu 74%) ya jumla ya watu milioni 48 ulimwenguni waliokimbia makazi yao wanaishi katika nchi 10 tu.[41]

Kwa mujibu wa kiwango cha idadi ya watu kitaifa, Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, ambayo vita vyake vimeendelea kwa zaidi ya mwongo mmoja, ilikuwa na zaidi ya asilimia 35 ya idadi ya watu wake waliofurushwa kutoka kwa makazi yao kwa sababu ya vita na vurugu. Somalia ilikuwa na kiwango cha pili cha juu zaidi (19%), ikifuatwa na Jamhuri ya Afrika ya Kati, Sudan Kusini na Yemen (zikiwa na zaidi ya 12%). Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba hasa kwa visa vya ufurushwaji vilivyochukua muda mrefu kusuluhishwa, kama vile huko Colombia, baadhi ya watu ambao wamerudi kwenye maeneo yao ya asili na kwenye nyumba zao bado wanaweza kuhesabiwa kama wakimbizi wa ndani. Hii ni kwa sababu, katika hali zingine, suluhisho la kudumu halijapatikana.[42] Mashirika kama vile IDMC hufuata mfumo wa Kamati ya Kudumu kati ya Mashirika kuhusu Suluhisho la Kudumu kwa Wakimbizi wa Ndani, ambalo linaweka vigezo vinane ambavyo vinatoa suluhisho la kudumu katika kuamua wakati watu hawapaswi kuchukuliwa tena kuwa wakimbizi wa ndani.[43]

39 IDMC inaangazia changamoto zilizopo katika kukusanya data za watu waliofurushwa kutokana na miradi ya maendeleo, ghasia za uhalifu au maafa yanayoanza taratibu, pamoja na jitihada zao za kuyashinda matatizo haya. Tazama IDMC, 2019:72–73.


40 IDMC, 2020:4.

41 Nchi hizo 10 zinajumuisha Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Colombia, Yemen, Afghanistani, Somalia, Nigeria, Sudan, Ethiopia na Sudan Kusini.

42 Suluhu ya kudumu hupatikana "wakati IDPs hawana tena usaidizi maalumu na mahitaji ya ulinzi ambayo yanahusishwa na kufurushwa kwao na watu kama hao wanaweza kufurahia haki zao za kibinadamu bila ubaguzi unaotokana na ufurushwaji wao." Tazama, kwa mfano, Taasisi ya Brookings na Chuo Kikuu cha Bern, 2010.

43 Vigezo hivyo vinajumuisha: usalama na ulinzi; kiwango cha kutosha cha maisha; upatikanaji wa riziki; urejeshaji wa makazi, ardhi ma mali; upatikanaji wa hati; kuunganishwa kwa familia; kushiriki katika masuala ya umma; na upatikanaji wa suluhu zinazofaa na haki. Tazama, kwa mfano, Taasisi ya Brookings na Chuo Kikuu cha Bern, 2010; IDMC, 2019.

Kielelezo cha 18. Nchi 20 zinazoongoza kwa idadi kubwa zaidi ya wakimbizi wa ndani kutokana na vita na vurugu mwishoni mwa 2020, milioni




*Chanzo:* IDMC, 2021.
*Maelezo:* Idadi ya IDP inarejelea kusanyiko la idadi ya watu waliofurushwa kwa muda mrefu. Wingi wa idadi ya watu uliotumika kukokotoa asilimia ya idadi ya IDP waliokumbwa na machafuko inategemea jumla ya idadi ya wakazi wa nchi kwa makadirio ya watu ya UN DESA (2021a).

Katika mwaka wa 2020, jumla ya idadi ya watu duniani waliohamishwa na maafa ilikuwa karibu watu milioni 7 katika nchi na maeneo 104. Iliripotiwa kuwa watu hawa walikuwa bado wanaishi mbali na makazi yao wakiwa wamefurushwa kufikia mwisho wa 2020 kutokana na maafa yaliyotokea katika mwaka wa 2020. Kama iliyobainishwa na IDMC, takwimu hii "si ya uhakika sana", kwa kuwa haijumuishi wale waliohamishwa na maafa ambayo yalitokea kabla ya 2020.

### Takwimu za IDP: mapendekezo

Mapendekezo mapya[a] yalichapishwa Januari 2021 na Kundi la Wataalamu wa Takwimu za Wakimbizi na IDP (EGRIS), ambalo lilianzishwa mwaka wa 2016 ili kuwezesha ukusanyaji wa takwimu rasmi za wakimbizi, waomba hifadhi na wakimbizi wa ndani. Mapendekezo hayo yamesasisha ripoti ya kiufundi ya 2018,[b] viwango vya kwanza vinavyotambulika duniani kote vya takwimu rasmi kuhusu ufurushwaji wa lazima, vikitoa mapendekezo kuhusu uzalishaji na usambazaji wa takwimu za ufurushwaji wa ndani. Ripoti ya Kundi la Wataalamu inajumuisha sura sita (ukiondoa utangulizi na tanbihi):

- **Mifumo na ufafanuzi wa kisheria na kisera**: viwango vya kimataifa na kikanda vya kulinda IDPs, na fafanuzi zisizo za kitakwimu zinazotumika kurejelea IDPs;
- **Mfumo wa kitakwimu wa ufurushwaji wa ndani**: uelezaji bayana wa vikundi vya watu katika upeo wa mapendekezo, na ufafanuzi wa takwimu za IDP wanaoingia mahali, idadi na wanaoondolewa mahali;
- **Suluhu za kudumu na hali ngumu kuu inayohusiana na ufurushwaji**: uchanganuzi wa hali ngumu ya IDP na tathmini ya maendeleo kuelekea kwa suluhu za kudumu;
- **Muhtasari wa vigeu na viashiria muhimu**: vigeu vilivyopendekezwa vikijumuisha umri na jinsia, na upangaji wa kategoria mbalimbali za watu ambao wako katika mfumo wa kitakwimu wa ufurushwaji wa ndani;
- **Vyanzo vya data kwa ajili ya kukusanya takwimu za IDPs**: vyanzo vya data, ikiwa ni pamoja na sensa na savei, zinazopatikana ili kutoa takwimu za IDP, na changamoto na faida zake; na
- **Kanuni na taratibu za uratibu wa takwimu za IDP**: viwango vya ubora na jukumu la uratibu juu ya data ya uendeshaji na kuimarisha mifumo ya takwimu kuhusu ufurushwaji wa lazima.

Mapendekezo yataendelea kutekelezwa na kundi la nchi zenye usaidizi wa kiufundi kutoka kwa wanachama wa EGRIS ili kujenga mifumo ya data na uwezo wa takwimu.

a EGRIS, 2020.
b EGRIS, 2018.

### *Ufurushwaji Mpya katika mwaka wa 2020*

Kufikia mwishoni mwa 2020, kulikuwa na jumla ya ufurushwaji mpya wa ndani milioni 40.5 katika nchi na maeneo 42 kutokana na vita na vurugu, na nchi na maeneo 144 kutokana na majanga. Asilimia sabini na sita (milioni 30.7) ya ufurushwaji huo mpya ulisababishwa na majanga na asilimia 24 (milioni 9.8) ulisababishwa na vita na vurugu.[44]


Katika mwaka wa 2020, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (milioni 2.2) na Jamhuri ya Kiarabu ya Syria (milioni 1.8) ziliongoza orodha hiyo na idadi kubwa zaidi ya ufurushwaji mpya uliosababishwa na vita na vurugu, na matokeo haya yakaathiri kwa kiasi kikubwa idadi ya waliofurushwa upya ulimwenguni. Nchi hizo zilifuatwa na Ethiopia (milioni 1.7), Msumbiji (milioni 0.6) na Burkina Faso (milioni 0.5). Ufilipino ilikumbwa na idadi kubwa zaidi ya watu waliofurushwa kutokana na majanga katika mwaka wa 2020 (takriban milioni 5.1).[45]

44 Yaliyomo katika kifungu hiki kidogo yamejikita katika na kutolewa katika IDMC, 2020, 2021. Tafadhali rejelea hati hizi kwa maelezo ya kiufafanuzi, uchanganuzi wa kina, tahadhari, vikwazo na mbinu zinazohusiana na namba na mienendo iliyowasilishwa. Ripoti za awali za IDMC *Global Estimates* (zinapatikana katika www.internal-displacement.org/global-report/), pamoja na Hifadhidata ya Ufurushwaji wa Ndani Duniani (IDMC, n.d.), ni vyanzo vingine vya taarifa.

45 IDMC inaangazia sababu zinazoweza kusababisha mabadiliko haya, ikijumuisha uimarishaji wa matukio ya mstari wa mbele ya vita, usitishaji mapigano, vikwazo vya uhuru wa kwenda popote na mabadiliko ya mbinu za ukusanyaji data.

Katika mwaka wowote ule, watu wengi zaidi hufurushwa kutoka kwa makazi yao na majanga kuliko wale wanaofurushwa upya na vita na vurugu, na nchi nyingi zaidi zimeathiriwa na ufurushwaji unaoletwa na majanga. Hili linabainika wakati wa kuchunguza idadi ya nchi na maeneo ambamo ufurushwaji mpya ulitokea katika mwaka wa 2020: 144 kutokana na majanga, ikilinganishwa na 42 kutokana na vita na vurugu (tazama Kielelezo cha 19). Kama ilivyokuwa katika miaka iliyotangulia, majanga yanayohusiana na hali ya anga yalisababisha idadi kubwa (milioni 30) ya wafurushwaji wapya, huku dhoruba zikisababisha watu milioni 14.6 kuyahama makazi yao na mafuriko kusababisha milioni 14.1.

Kielelezo cha 19. Ufurushwaji unaotokana na vita (juu) na ufurushwaji unaotokana na majanga (chini) mnamo 2020 kieneo




*Chanzo*: IDMC, 2021.

*Maelezo*: Ramani hii inatumiwa kama kielelezo tu. Mipaka na majina yaliyoonyeshwa na maelezo yaliyotumika kwenye ramani hii hayamaanishi kuwa imeidhinishwa rasmi au kukubaliwa na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji.

Kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo cha 20, katika miaka iliyopita, idadi ya watu wapya waliofurushwa na majanga kila mwaka ilizidi idadi ya watu waliofurushwa na vita na vurugu. Hayta hivyo, IDMC inabainisha kwamba sehemu kubwa ya jumla ya kimataifa ya ufurushwaji mpya inayotokana na majanga kwa kawaida huhusishwa na uokoaji wa muda mfupi kwa njia salama na yenye utaratibu.

Kielelezo cha 20. Ufurushwaji mpya wa ndani unaosababishwa na vita na majanga, 2010–2020 (milioni)




*Chanzo:* IDMC, n.d. (ilisomwa Mei 2021).

*Maelezo:* Istilahi "ufurushwaji mpya" inarejelea idadi ya harakati za kufurushwa ambazo zilitokea katika mwaka mahususi, si jumla ya idadi ya IDP waliokusanyika wanaotokana na kufurushwa kwa muda mrefu. Takwimu mpya za ufurushwaji zinajumuisha watu ambao wamefurushwa zaidi ya mara moja, na hazilingani na idadi ya watu waliofurushwa katika mwaka fulani.

### Matriki ya IOM ya Ufuatiliaji wa Ufurushwaji

Programu ya Matriki ya IOM ya Ufuatiliaji na Ufurushwaji (DTM) hukusanya na kuchanganua data ili kusambaza taarifa muhimu za safu nyingi kuhusu ufurushwaji na mwendo wa watu. Ukusanyaji na uchanganuzi wa data wa DTM huwawezesha watoa maamuzi na watoa majibu kuwapa watu hawa usaidizi bora zaidi wa muktadha mahususi na unaotegemea ushahidi. Data zinashirikishwa kwa njia ya ramani, michorotaarifa, ripoti, taswira zinazoingiliana za wavuti, na usariifishaji wa data ghafi au iliyoboreshwa. Kulingana na muktadha uliotolewa, DTM hukusanya habari juu ya idadi ya watu, maeneo, hali, mahitaji na hali ngumu, ikitumia zana moja au zaidi ya zifuatazo za kimethodolojia:

- Kufuatilia uhamaji na mahitaji ya sekta nyingi katika maeneo maalumu ili kuelekeza msaada unapohitajika;
- Kufuatilia mienendo ya uhamaji ("mtiririko") na hali ya jumla katika vituo vya asili, mpito na wanakokwenda;
- Kuwasajili watu binafsi na kaya kwa uteuzi wa wanufaishwa, kulenga walio hatarini na upangaji;
- Kufanya utafiti, ili kukusanya habari za kina kutoka kwa watu wanaohusika.

Katika mwaka wa 2020, ikifanya kazi katika zaidi ya nchi 80, DTM ilifuatilia zaidi ya IDP milioni 30, waliorejea milioni 26 na wahamiaji milioni 5. Data za DTM ya IOM ni mojawapo ya vyanzo vikubwa zaidi vya makadirio ya kila mwaka ulimwenguni juu ya ufurushwaji wa ndani vilivyotayarishwa na IDMC. Kwa taarifa zaidi kuhusu DTM ya IOM, tazama http://dtm.iom.int.

## Hitimisho

Ni muhimu kuelewa uhamiaji na ufurushwaji, na jinsi unavyobadilika ulimwenguni, ukizingatia umuhimu wake kwa Mataifa, jamii za maeneo mahususi na watu binafsi. Huenda uhamiaji na usafiri wa binadamu ni mambo ya zamani ambayo yanarudi nyuma hadi vipindi vya mwanzo vya historia, lakini udhihirikaji na athari zake zimebadilika katika kipindi cha muda mrefu kwani ulimwengu umekuwa wa utandawazi zaidi.[46] Hili limeangaziwa kwa uwazi zaidi huku UVIKO-19 ikiendelea kutatiza kwa kiasi kikubwa uhamiaji na usafiri wa kimataifa (na Nyanja nyingine nyingi za jamii ya kisasa), zaidi ya miezi 18 tangu ilipotangazwa kwa mara ya kwanza na WHO kuwa ugonjwa tandavu.[47] Vikwazo vinavyoendelea vya usafiri vinasalia kuwa kipengele muhimu katika jamii nyingi ulimwenguni wakati aina za virusi zikisababisha visa vilivyothibitishwa kuongezeka tena na huku utoaji wa chanjo ukiendelea, ingawa kwa njia isiyo na utaratibu duniani kote. Vikwazo vya usafiri – vya kimataifa na vya ndani – viliibuka kama nguzo moja kuu ya kukabiliana na UVIKO-19 na, wakati vikigeuka na kubadilikabadilika, vimeendelea kuwepo tangu wakati huo. Sura ya mada kuhusu athari za UVIKO-19 (Sura ya 5 ya ripoti hii) inachunguza masuala haya kwa undani zaidi, kwa kuzingatia miezi 12 ya kwanza ya ugonjwa huu tandavu na athari zake za muda mrefu.

Sasa, zaidi ya wakati mwingine wowote katika historia, tuna habari zaidi juu ya uhamiaji na ufurushwaji kwa matumizi yetu; na bado, hali ya uhamiaji katika ulimwengu uliounganishwa inamaanisha kuwa inaweza kuwa vigumu kunasa

46 McAuliffe na Goossens, 2018; Triandafyllidou, 2018.
47 WHO, 2020.

michakato yake katika takwimu. Baada ya kusema hayo, tumeona seti mpya kabisa za data zikiibuka haraka sana wakati wa ugonjwa huu tandavu, ikijumuisha ile iliyotoka kwa IOM (Kielelezo cha 8) na mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa, na vilevile kutoka taasisi za kiakademia.[48] Zaidi ya hayo, baadhi ya makampuni makubwa ya teknolojia, ikiwa ni pamoja na Facebook na Google, yalianza kutoa data isiyotaja chanzo ugonjwa huu tandavu ulipoanza ambayo ilitokana na rekodi za usafiri wa watumiaji, ikitoa dalili ya kiasi kikubwa cha data ya kurekodiwa iliyokusanywa, huku pia ikisisitiza wasiwasi uliopo kuhusu athari kwa haki za binadamu (pamoja na faragha) za hifadhi hizo za data na matumizi yake.[49] Pia tunaona jinsi ongezeko la udijitishaji wa uhamiaji na usafiri – ambavyo msingi wake ni data – unavyozidi kutumiwa kama sehemu ya juhudi zinazoendelea za kukuza na kutekeleza teknolojia ya akili tarakilishi katika mifumo ya uhamiaji (tazama Sura ya 11 ya ripoti hii). Upunguzaji wa ukosefu wa usawa duniani pia unasaidiwa na ukusanyaji na uchambuzi wa data. Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji Salama Uliopangwa na Halali unasisitiza ahadi ya kuboresha ushirikiano wa kimataifa kuhusu uhamiaji, pamoja na kukusanya data ya uhamiaji na kufanya utafiti na uchanganuzi ili tuweze kuelewa vyema zaidi mienendo na ruwaza na michakato inayojitokeza, ili kusaidia ukuzaji wa mwitikio uliojikita kwenye ushahidi. Matukio ya hivi majuzi katika eneo hili yamefafanuliwa katika Sura ya 4, yakirejelea hasa kazi inayofanywa na Mtandao wa Umoja wa Mataifa kuhusu Uhamiaji.

Katika muktadha wa utandawazi unaoendelea, pamoja na kupanua ukusanyaji wa data na michakato inayohusiana na udigitishaji, inafaa zaidi kufahamu vyema mienendo ya muda mrefu na ruwaza zinazobadilika katika uhamiaji na ufurushwaji. Katika sura hii, tumetoa muhtasari wa hali iivyo duniani kuhusu uhamiaji na wahamiaji, kulingana na data iliyopo sasa. Licha ya mapengo na ucheleweshaji wa data, mahitimisho kadhaa ya kiwango cha juu yanaweza kutolewa. Katika ngazi ya kimataifa, kwa mfano, tunaweza kuona kwamba, baada ya muda, wahamiaji wamepata makazi katika baadhi ya kanda (kama vile Asia na Ulaya) kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko zingine (kama vile Afrika na Amerika ya Kusini na Karibiani); na kwamba kuna uwezekano wa hali hii kuendelea kwa muda mrefu, licha ya athari kubwa za ugonjwa huu tandavu katika miezi ya hivi karibuni. Kadhalika, takwimu zinaonyesha kwamba wafanyikazi wahamiaji wanaendelea kushawishika kuelekea kwenye maeneo yenye fursa nyingi, jinsi uchumi unavyokua na soko la ajira linavyobadilika, na kwamba baadhi ya makundi ya wafanyikazi wahamiaji yanaegemea sana jinsia moja (tazama Kielelezo cha 11). Baada ya kusema hayo, uchanganuzi wa ziada katika ripoti hii (Sura ya 7) unaonyesha kwamba kumekuwepo na mabadiliko katika kile kinachounda njia za uhamiaji, pamoja na ishara kwamba uhamaji mkubwa umekuwa ukitokea kutoka nchi zilizoendelea sana katika miaka ya hivi karibuni.

Data za ulimwengu pia zinaonyesha kuwa ufurushwaji unaosababishwa na vita, vurugu za jumla na mambo mengine bado ni wa juu sana, licha ya ugumu wa ziada wa kukusanya data wakati wa ugonjwa huu tandavu. Vita na vurugu zisizodhibitiwa kwa urahisi, zisizotatuliwa na za mara kwa mara zimesababisha kuongezeka kwa idadi ya wakimbizi duniani kote. Wakati nchi chache zinaendelea kutoa suluhisho kwa wakimbizi, kwa jumla, hizi hazitoshi kushughulikia mahitaji ya ulimwengu mzima. Zaidi ya hayo, ilikadiriwa kwamba kulikuwa na watu wengi waliokimbia makazi yao ndani ya nchi mwishoni mwa 2020 kuliko hapo awali. Matukio ya hivi majuzi ya kusikitisha nchini Afghanistani yanaonyesha kuwa kuna uwezekano wa kuona idadi ya watu waliofurushwa makwao duniani ikiongezeka zaidi katika siku za usoni kadri watu wanavyofurushwa ndani na kutoka nchi hiyo katika kipindi kilichosalia cha 2021 na hadi 2022.

48 Tazama, kwa mfano, Kifuatiliaji cha Mwitikio wa Serikali cha Chuo Kikuu cha Oxford (kilichotumika katika sura hii) na seti ya data ya UVIKO-19 ya Chuo Kikuu cha John Hopkins (inayorejelewa katika Sura ya 5 ya ripoti hii).

49 Toh, 2020; Zuboff, 2021.

## Kiambatisho A. Dondoo lililofupishwa: *Ripoti ya Mwisho kuhusu Mifumo ya Dhanifu na Dhana na Ufafanuzi kuhusu Uhamiaji wa Kimataifa* (27 Aprili 2021)

Ripoti kamili inapatikana katika https://unstats.un.org/unsd/demographic-social/migration-expert-group/task-forces/TF2-ConceptualFramework-Final.pdf.

*Utangulizi na Usuli*

1. Kitengo cha Takwimu cha Umoja wa Mataifa, chini ya uelekezi wa Kundi la Wataalamu la Umoja wa Mataifa kuhusu Takwimu za Uhamiaji, kimeanzisha marekebisho ya Mapendekezo ya 1998 kuhusu Takwimu za Uhamiaji wa Kimataifa (yanayorejelewa baadaye kama Mapendekezo ya 1998). Hadi sasa, ufafanuzi wa mhamiaji wa kimataifa kama ulivyoelezwa katika Mapendekezo ya 1998 umeleta kiwango fulani cha ulinganifu katika nchi zote. Hata hivyo, zaidi ya miaka 20 imepita tangu Mapendekezo ya 1998 kuchapishwa. Hadi kutokea kwa ugonjwa tandavu wa UVIKO-19 mnamo 2020, vikwazo vya uhamiaji wa kimataifa vilipunguzwa. Hususan, teknolojia za kisasa za mawasiliano na ongezeko la urahisi wa kusafiri vilipunguza mzigo wa kisaikolojia wa kuishi katika nchi zingine kwa kuwa wahamiaji waliweza kuendelea kuwasiliana mara kwa mara na familia na marafiki zao walio katika nchi zao za asili. Hii inajumuisha hatua za muda na za kudumu zinazohusiana na elimu au nafasi za kazi na zile zinazotokana na hali ya kisiasa au mazingira. Pia makubaliano ya kikanda yamefikiwa ambayo yanatoa uhuru wa kuingia na kutoka miongoni mwa nchi fulani, na kuibua changamoto mpya za kupima hata kwa nchi zilizo na mifumo iliyoendelea ya takwimu.

2. Kuongezeka kwa viwango na ruwaza za mabadiliko ya uhamiaji wa kimataifa, pamoja na wanaotafuta hifadhi na wakimbizi, kumeongeza mahitaji ya data sahihi na inayopatikana kwa wakati. Wito wa data bora kutoka kwa mipango mbalimbali imesisitiza haja ya kukusanya na kutumia takwimu za uhamiaji ili kutayarisha sera za uhamiaji zilizojikita kwenye ushahidi na kuongoza ujumuishaji wa wahamiaji katika mipango ya maendeleo ya kitaifa. Data hizi zinahitajika pia kwa ukadiriaji wa idadi ya watu na kuelewa mabadiliko ya kidemografia. Huku kukiwa na ongezeko la miaka ambayo mtu anatarajiwa kuishi na kupungua kwa uzazi katika nchi nyingi duniani, uhamiaji umekuwa sehemu muhimu ya mabadiliko ya kidemografia na kijamii.

3. Data bora na inayotolewa kwa wakati kuhusu uhamiaji wa kimataifa inahitajika kwa sababu nyingi. Data hii huhusiana zaidi na ukuaji au upunguaji wa idadi ya watu, maendeleo ya kiuchumi na matatizo ya kimazingira. Kwa mfano, wahusika wa maeneo mahususi huhitaji hesabu za watu wanaotumia huduma za maeneo hayo (k.m. makazi, afya, na huduma za kijamii, shule), wakati huenda wadau wa kitaifa wakavutiwa zaidi na ukubwa, sifa na mtawanyiko wa wahamiaji katika eneo lote la kitaifa ili kutathmini athari yake kwa mabadiliko ya idadi ya watu na soko la ajira ya ndani. Kwa vile uhamaji wa kimataifa unahusisha usafiri wa watu kutoka nchi moja hadi nyingine, kuna haja ya kubadilishana data kuhusu safari hizi na kuhakikisha kwamba zinalinganishwa kwa muda mrefu. Bila data kama hiyo, haiwezekani kukadiria ukubwa wa watu wanaoishi nje ya nchi au kutathmini ukubwa na sifa za idadi na mtiririko wa uhamiaji wa kimataifa. Wala haiwezekani kutimiza mahitaji ya data ya Mkataba wa Ulimwengu wa Umoja wa Mataifa wa Uhamiaji Salama, Uliopangwa na Halali na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Wakati nchi nyingi zikitatizika kukusanya takwimu za mienendo ya watu, kuwa na utaratibu wa kujenga uwezo katika maendeleo na uboreshaji wa takwimu za uhamiaji kunaweza kuwa kwa manufaa sana.

### *Kufikiria upya kuhusu Uhamiaji na Usafirii wa Kimataifa*

17. Katika sehemu hii, tunatoa muhtasari wa mfumo dhanifu wa usafiri na uhamiaji wa kimataifa. Usafiri wa kimataifa unajumuisha mwendo wowote ambao unavuka mipaka ya kimataifa katika mwaka fulani. Uhamiaji wa kimataifa unafafanuliwa kwa ufupi zaidi kama kubadilisha nchi ya makazi na unachukuliwa kuwa sehemu ndogo ya usafiri wa kimataifa. Mitiririko hii ni muhimu katika kuelewa mabadiliko ya idadi ya wakazi, ambayo ndiyo idadi kuu ya watu inayotumiwa katika ulinganishaji wa kimataifa. Katika mfumo wetu dhanifu, tunagawa idadi ya watu na kundi linalohusiana nayo linalosafiri kimataifa katika vikundi viwili tofauti: (i) idadi ya wakazi na uhamiaji wa kimataifa na (ii) idadi ya watu wa muda (wasio wakazi) na usafiri wa muda wa kimataifa. Usafiri wa muda wa kimataifa unajumuisha kuvuka mipaka ya kimataifa (matukio) isipokuwa ile inayohusiana na mabadiliko katika idadi ya wakazi.

18. Tunafafanua makazi kulingana na Kanuni na Mapendekezo ya Umoja wa Mataifa kwa Sensa za Watu na Makazi (Rekebisho la 3, aya 2.50). Hii ina maana kuwa inapendekezwa kwamba nchi zitumie kipimo cha miezi 12 wakati wa kufikiria juu ya makazi yake mtu kulingana na mojawapo ya vigezo viwili vifuatavyo:


    a. Mahali ambapo mtu huyo ameishi mfululizo kwa muda mwingi wa miezi 12 iliyopita (yaani, kwa angalau miezi 6 na siku moja), bila kujumiuisha kutokuwepo kwa muda  kwa sababu ya likizo au shughuli za kikazi, au anakusudia kuishi kwa angalau miezi 6 na siku moja;

    b. Mahali ambapo mtu huyo ameishi mfululizo kwa angalau miezi 12 iliyopita, bila kujumisha kutokuwepo kwa muda kwa sababu ya likizo au shughuli za kikazi, au anakusudia kuishi kwa angalau miezi 12.

…

27. Katika Kielelezo cha 2, tunawasilisha mfumo dhanifu unaounganisha wanaowasili kimataifa na watu waliopo sasa, ambao wanajumuisha watu wote walio nchini wakati fulani, bila kujumuisha wakazi walio nje ya nchi kwa muda. JJambo kuu linalotofautisha uhamiaji wa kimataifa na safari zingine za watu kimataifa ni muda wanaokaa nchini au nje ya nchi. Kwa hivyo, kigezo cha kufafanua mhamiaji kinapaswa kuwa muda unaohitajika ili kuchukuliwa kuwa mmoja wa wakazi wa sehemu hiyo. Kiutendaji, hii inaweza kumaanisha muda wa miezi 6 au miezi 12 (tazama aya ya 18) ili mtiririko wa uhamiaji ulingane na mabadiliko ya kila mwaka ya wakazi. Hali ni kama hiyo kwa wanaoondoka: watu wanahitaji kutokuwepo na kuishi katika nchi nyingine kwa muda wa kutosha kulingana na mahitaji ya chini sana ya makazi ili wafikiriwe kuwa sehemu ya wakazi wa nchi hiyo nyingine. Watu ambao waliishi kwa muda mfupi katika zaidi ya nchi moja kwa muda usiotimiza vigezo vilivyowekwa hawawezi kuanzisha makazi mapya, kwa hivyo bado wao ni sehemu ya wakazi wa nchi zao za asili. Katika mfumo huu, tunajumuisha watu ambao hawajawahi kuwa sehemu ya wakazi. Pia tunajumuisha kubadilisha hadhi kwa idadi ya watu wa muda hadi idadi ya wakazi kwa watu ambao wanaishi kwa zaidi ya muda wa chini unaokubalika wa kigezo kilichowekwa wakiwa bado wapo nchini. Watu walioishi kwa muda mrefu zaidi ya vigezo vya muda na hawana visa halali au hati zingine za uhamiaji wanapaswa kuchukuliwa kuwa sehemu ya wakazi.

## Kielelezo cha 2. Mfumo dhanifu kuhusu makutanio kati ya muda wa kukaa na usafiri wa kimataifa



# Marejeo*

*Al Jazeera*
2020 Coronavirus: Travel restrictions, border shutdowns by country. 3 June. Inapatikana www.aljazeera.com/news/2020/6/3/coronavirus-travel-restrictions-border-shutdowns-by-country.

Amuedo-Dorantes, C.
2014 The good and the bad in remittance flows. *IZA World of Labor*. Inapatikana https://wol.iza.org/articles/good-and-bad-in-remittance-flows/long.

Aron, J. na J. Muellbauer
2019 *The Economics of Mobile Money: Harnessing the Transformative Power of Technology to Benefit the Global Poor.* Oxford Martin School, University of Oxford. Inapatikana www.oxfordmartin.ox.ac.uk/publications/mobile-money.

Benton, M., J. Batalova, S. Davidoff-Gore na T. Schmidt
2021 *COVID-19 and the State of Global Mobility in 2020*. Migration Policy Institute Europe, Brussels. Inapatikana www.migrationpolicy.org/research/covid-19-state-global-mobility-2020.

Brookings Institution na University of Bern
2010 *IASC Framework on Durable Solutions for Internally Displaced Persons*. Brookings Institution, Washington, D.C. Inapatikana www.unhcr.org/50f94cd49.pdf.

de Beer, J., J. Raymer, R. van der Erf na L. van Wissen
2010 Overcoming the problems of inconsistent international migration data: A new method applied to flows in Europe. *European Journal of Population*, 26(4):459–481.

Dinarte, L., D. Jaume, E. Medina-Cortina na H. Winkler
2021 *Not by Land nor by Sea: The Rise of Formal Remittances during COVID-19.* Development Policy Centre, Australian National University, Canberra. Inapatikana https://devpolicy.org/Events/2021/Not-by-land-nor-by-sea-the-rise-of-formal-remittances-during-COVID-19-Dinarte-13Apr/full-paper-updated13Apr.pdf.

Eurostat
2020 Personal Remittances Statistics. Inapatikana https://ec.europa.eu/eurostat/statistics-explained/index.php?title=Personal_remittances_statistics (accessed 2 June 2021).

Expert Group on Refugee and IDP Statistics (EGRIS)
2018 Technical report on statistics of Internally Displaced Persons. Inapatikana https://ec.europa.eu/eurostat/web/products-manuals-and-guidelines/-/ks-gq-18-003.

2020 International recommendations on Internally Displaced Persons Statistics (IRIS). Inapatikana https://ec.europa.eu/eurostat/web/products-manuals-and-guidelines/-/ks-gq-20-005.

Fertig, M. na C.M. Schmidt
2001 First- and second-generation migrants in Germany – What do we know and what do people think? *IZA Discussion Papers*, 286:1–48. Inapatikana www.iza.org/publications/dp/286/first-and-second-generation-migrants-in-germany-what-do-we-know-and-what-do-people-think.

* Viungo wavuti vyote vilikuwa vikifanya kazi wakati wa kuandika ripoti hii.

Gallagher, A. na M. McAuliffe

2016 South-East Asia and Australia. In: *Migrant Smuggling Data and Research: A Global Review of the Emerging Evidence Base* (M. McAuliffe and F. Laczko, eds.). IOM, Geneva. Inapatikana https://publications.iom.int/system/files/smuggling_report.pdf.

Ghosh, B.

2006 *Migrants' Remittances and Development: Myths, Rhetoric and Realities*. IOM, Geneva. Inapatikana https://publications.iom.int/es/books/migrants-remittances-and-development-myths-rhetoric-and-realities (accessed 2 June 2021).

Hale, T., S. Webster, A. Petherick, T. Phillips na B. Kira

2021 *Oxford COVID-19 Government Response Tracker Dataset*, Blavatnik School of Government, Oxford. (accessed 3 June 2021) Inapatikana https://covidtracker.bsg.ox.ac.uk/.

International Civil Aviation Organization (ICAO)

2021 *Effects of Novel Coronavirus (COVID-19) on Civil Aviation: Economic Impact Analysis*. ICAO, Montreal. Inapatikana www.icao.int/sustainability/Documents/Covid-19/ICAO_coronavirus_Econ_Impact.pdf.

Internal Displacement Monitoring Centre (IDMC)

2019 *Global Report on Internal Displacement 2019*. Geneva. Inapatikana www.internal-displacement.org/global-report/grid2019/.

2020 *Global Report on Internal Displacement 2020.* Geneva. Inapatikana www.internal-displacement.org/global-report/grid2020/.

2021 *Global Report on Internal Displacement 2021.* Geneva. Inapatikana www.internal-displacement.org/global-report/grid2021/.

n.d. Global Internal Displacement Database. Inapatikana www.internal-displacement.org/database (accessed 3 June 2021).

International Labour Organization (ILO)

2018 *ILO Global Estimates on International Migrant Workers – Results and Methodology.* Second edition. Geneva. Inapatikana www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---dgreports/---dcomm/---publ/documents/publication/wcms_652001.pdf.

2021 *ILO Global Estimates on International Migrant Workers – Results and Methodology.* Third edition. Geneva. Inapatikana www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---dgreports/---dcomm/---publ/documents/publication/wcms_808935.pdf.

International Monetary Fund (IMF)

2020 Supporting migrants and remittances as COVID-19 rages on. *IMF Blog*, 11 September. Inapatikana https://blogs.imf.org/2020/09/11/supporting-migrants-and-remittances-as-covid-19-rages-on/.

International Organization for Migration (IOM)

2020a World Migration Report 2020 Interactive. Geneva. Inapatikana https://worldmigrationreport.iom.int.

2020b Global Mobility Restrictions Update. Inapatikana https://migration.iom.int/system/tdf/reports/DTM-Covid19%20Global%20Overview%20Output%2019.03.2020%20_0.pdf?file=1&type=node&id=7977.

2020c *COVID-19 Impact on Stranded Migrants*. COVID-19 Response, Return Task Force. Geneva. Inapatikana www.iom.int/sites/default/files/documents/issue_brief_return_task_force.pdf.

2020d *Return and Reintegration Quarterly Bulletin – 2020 Q1*. Geneva. Inapatikana www.iom.int/sites/default/files/our_work/DMM/AVRR/2020q1-returnandreintegrationquarterlybulletin.pdf.

2020e *Return and Reintegration Quarterly Bulletin – 2020 Q2*. Geneva. Inapatikana www.iom.int/sites/default/files/our_work/DMM/AVRR/2020q2-returnandreintegrationquarterlybulletin.pdf.

2020f *Return and Reintegration Quarterly Bulletin – 2020 Q3*. Geneva. Inapatikana www.iom.int/sites/default/files/our_work/DMM/AVRR/2020q3-returnandreintegrationquarterlybulletin.pdf.

2020g *COVID-19 Analytical Snapshot #16: International Remittances*. 17 April. Geneva. Inapatikana www.iom.int/sites/default/files/documents/covid-19_analytical_snapshot_16_-_international_remittances.pdf.

2020h *COVID-19 Analytical Snapshot #53: International Remittances UPDATE*. 26 August. Geneva. Inapatikana www.iom.int/sites/default/files/documents/covid-19_analytical_snapshot_53_-_international_remittances_update.pdf.

2020i *COVID-19 Analytical Snapshot #55: Emerging Remittance Patterns*. 15 October. Geneva. Inapatikana www.iom.int/sites/default/files/documents/covid-19_analytical_snapshot_55_-_emerging_remittance_patterns_0.pdf.

2020j IOM Resettlement. Inapatikana https://publications.iom.int/system/files/pdf/resettlement-booklet-2020.pdf.

2021a Travel Restrictions Matrix. Inapatikana https://migration.iom.int/sites/all/themes/fmp/pages/heatmap/matrix.php.

2021b *COVID-19 Analytical Snapshot #66: International Remittances UPDATE*. 25 January. Geneva. Inapatikana www.iom.int/sites/default/files/documents/covid-19_analytical_snapshot_66_international_remittances_update.pdf.

n.d. Latest Global Figures: Missing Migrants Project: Tracking Deaths Along Migratory Routes. Inapatikana https://missingmigrants.iom.int/ (accessed 20 September 2021).

Johns Hopkins Coronavirus Resource Centre (CRC)

2021 COVID-19 Dashboard. Inapatikana https://coronavirus.jhu.edu/map.html.

Koser, K.

2010 Dimensions and dynamics of irregular migration. *Population, Space and Place*, 16(3):181–193. Inapatikana https://onlinelibrary.wiley.com/doi/abs/10.1002/psp.587.

Kyaw, N.N.
2017 Unpacking the presumed statelessness of Rohingyas. *Journal of Immigrant and Refugee Studies*, 15(3):269–286.

McAuliffe, M., A. Kitimbo, A.M. Goossens na A.K.M. Ahsan Ullah
2017 Understanding migration journeys from migrants' perspectives. In: *World Migration Report 2018* (M. McAuliffe and M. Ruhs, eds.). IOM, Geneva. Inapatikana http://publications.iom.int/system/files/pdf/wmr_2018_en_chapter7.pdf.

McAuliffe, M. na A.M. Goossens
2018 Regulating international migration in an era of increasing interconnectedness. In: *Handbook of Migration and Globalisation* (A. Triandafyllidou, ed.). Edward Elgar Publishing, Cheltenham, pp. 86–104.

McAuliffe, M. na K. Koser
2017 Introduction. In: *A Long Way to Go: Irregular Migration Patterns, Processes, Drivers and Decision-making* (M. McAuliffe and K. Koser, eds.). ANU Press, Canberra.

McAuliffe, M.
2020 Immobility as the ultimate "migration disrupter". IOM Migration Research Series No. 64. 7 August. Inapatikana https://publications.iom.int/books/mrs-no-64-immobility-ultimate-migration-disrupter.

Neto, F.
1995 Predictors of satisfaction with life among second generation migrants. *Social Indicators Research*, 35:93–116.

Organisation for Economic Co-Operation and Development (OECD)
n.d.a International Migration Database. Inapatikana https://stats.oecd.org/Index.aspx?DataSetCode=MIG (accessed 2 September 2019).

n.d.b Foreign-Born Employment. Inapatikana https://data.oecd.org/migration/foreign-born-employment.htm (accessed 2 September 2019).

n.d.c Net ODA. Inapatikana https://data.oecd.org/oda/net-oda.htm (accessed 3 September 2019).

Poulain, M. na N. Perrin
2001 *Is the Measurement of International Migration Flows Improving in Europe*. Working Paper No. 12. Joint ECE–EUROSTAT Work Session on Migration Statistics organized in cooperation with the UN Statistics Division. UN Statistical Commission and the UN Economic Commission for Europe (Eurostat). Geneva, 21–23 May. Inapatikana www.unece.org/fileadmin/DAM/stats/documents/ece/ces/2001/05/migration/12.e.pdf.

Ratha, D., S. De, E.J. Kim, S. Plaza, G. Seshan na N.D. Yameogo
2020a *Migration and Development Brief 32: COVID-19 Crisis Through a Migration Lens*. KNOMAD, World Bank, Washington, D.C. Inapatikana www.knomad.org/publication/migration-and-development-brief-32-covid-19-crisis-through-migration-lens.

2020b *Migration and Development Brief 33: Phase II: COVID-19 Crisis Through a Migration Lens*. KNOMAD, World Bank, Washington, D.C. Inapatikana www.knomad.org/publication/migration-and-development-brief-33.

Ratha, D., E.J. Kim, S. Plaza na G. Seshan
2021 *Migration and Development Brief 34: Resilience: COVID-19 Crisis Through a Migration Lens*. KNOMAD, World Bank, Washington, D.C. Inapatikana www.knomad.org/publication/migration-and-development-brief-34.

Skeldon, R.
2018 International migration, internal migration, mobility and urbanization: Towards more integrated approaches. Migration Research Series, No. 53. IOM, Geneva. Inapatikana https://publications.iom.int/system/files/pdf/mrs_53.pdf.

Toh, A.
2020 Big data could undermine the COVID-19 response. *Wired*, 12 April. Inapatikana www.wired.com/story/big-data-could-undermine-the-covid-19-response/.

Triandafyllidou, A. (ed.)
2018 *Handbook of Migration and Globalization*. Edward Elgar Publishing, Cheltenham.

United Nations Department of Economic and Social Affairs (UN DESA)
1998 *Recommendations on Statistics of International Migration: Revision 1.* New York. Inapatikana https://unstats.un.org/unsd/publication/seriesm/seriesm_58rev1e.pdf.

2008 *International Migrant Stock: The 2008 Revision*. New York. Inapatikana https://esa.un.org/migration/index.asp?panel=1.

2015 *World Population Prospects: The 2015 Revision*. New York. Inapatikana https://esa.un.org/unpd/wpp/publications/files/key_findings_wpp_2015.pdf.

2021a *International Migrant Stock 2020.* New York. Inapatikana www.un.org/development/desa/pd/content/international-migrant-stock.

2021b *International Migrant Stock 2020 Documentation*. New York. Inapatikana www.un.org/development/desa/pd/sites/www.un.org.development.desa.pd/files/undesa_pd_2020_international_migrant_stock_documentation.pdf.

2021c *International Migration 2020 Highlights*. New York. Inapatikana www.un.org/development/desa/pd/sites/www.un.org.development.desa.pd/files/undesa_pd_2020_international_migration_highlights.pdf.

United Nations Development Programme (UNDP)
2009 *Human Development Report 2009*. New York. Inapatikana www.hdr.undp.org/sites/default/files/reports/269/hdr_2009_en_complete.pdf.

United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR)
2011 *Global Trends 2010*. Geneva. Inapatikana www.unhcr.org/4dfa11499.pdf#:~:text=Global%20Trends%202010.%20Global%20Trends%202010.%2060%20years.,at%20the%20end%20of%202010.%2012%20million%20stateless.

2021a *Global Trends: Forced Displacement in 2020*. Geneva. Inapatikana www.unhcr.org/flagship-reports/globaltrends/.

2021b *UNHCR Projected Global Resettlement Needs*. Geneva. Inapatikana www.unhcr.org/protection/resettlement/5ef34bfb7/projected-global-resettlement-needs-2021-pdf.html.

n.d.a Population Statistics. Inapatikana http://popstats.unhcr.org/en/persons_of_concern (accessed 23 June 2021).

n.d.b Resettlement. Inapatikana http://popstats.unhcr.org/en/resettlement (accessed 3 May 2021).

United Nations Statistical Commission

2021 *Report on the Fifty-second session of the Statistical Commission* (1–5 March 2021). New York. Inapatikana https://unstats.un.org/unsd/statcom/52nd-session/documents/2021-30-FinalReport-E.pdf.

United Nations Statistics Division

2021 *United Nations Expert Group on Migration Statistics, Task Force 2: Task force on Key Concepts and Definitions related to International Migration*. New York. Inapatikana https://unstats.un.org/unsd/demographic-social/migration-expert-group/task-forces/taskforce-2.

World Bank

2016 *Migration and Remittances Factbook 2016.* Third edition. Washington, D.C. Inapatikana https://openknowledge.worldbank.org/bitstream/handle/10986/23743/9781464803192.pdf?sequence=3&isAllowed=y.

2021a Defying predictions, remittance flows remain strong during COVID-19 crisis. May 12. Inapatikana www.worldbank.org/en/news/press-release/2021/05/12/defying-predictions-remittance-flows-remain-strong-during-covid-19-crisis.

2021b *Remittance Prices Worldwide Quarterly*. Issue 37. Washington, D.C. Inapatikana https://remittanceprices.worldbank.org/sites/default/files/rpw_main_report_and_annex_q121_final.pdf.

n.d. Migration and Remittances Data (updated as of May 2021). Inapatikana www.worldbank.org/en/topic/migrationremittancesdiasporaissues/brief/migration-remittances-data (accessed 3 June 2021).

World Health Organization (WHO)

2020 WHO Director-General's opening remarks at the media briefing on COVID-19. 11 March. Inapatikana: www.who.int/director-general/speeches/detail/who-director-general-s-opening-remarks-at-the-media-briefing-on-covid-19---11-march-2020.

Zuboff, S.

2021 The pandemic all but killed privacy. It's not too late to bring it back. Interview with Prof Soshanna Zuboff on *Marketplace* "Make me smart" podcast, episode 420, 27 April. Inapatikana www.marketplace.org/shows/make-me-smart-with-kai-and-molly/the-pandemic-all-but-killed-privacy-its-not-too-late-to-bring-it-back/.